# Nipashe

Jumatano Mei 6, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580224

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Watu 13 wafariki ajali za barabarani Pwani, Tanga

UK. 2



Upinzani majeruhi unapoingia mchakato uchaguzi mkuu

siasa

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe

Muungano unavyoboreka raia wataupenda zaidi

Balozi Mahiga: Lulu iliyoondoka

UKURASA 11

# Agizo la Mbowe latikisa Chadema

**KATIBU** wa wabunge aachia ngazi, Mnadhimu Upinzani ahusishwa ...*Endelea ukurasa 2*



Katibu wa Wabunge wa Chadema, David Silinde (Kulia) na Mnadhimu Mkuu Kambi ya Upinzani, Ester Bulaya.

## BAA LA CORONA



Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), utafiti unaonyesha watoto na vijana wako kwenye hatari ya kundi la kusambaza ugonjwa wa Covid-19, hivyo wanatakiwa kujilinda.

- Epuka mikusanyiko ya watu
- Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka
- Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana
- Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo

## MAGONJWA YANAYOUA WABUNGE KUTOTAJWA

UKURASA 2

**RIPOTI MAALUM - 3**

# Hii ndiyo hatima ya korosho msimu huu

UK. 4




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


**MICHEZO** TFF YAZIONYA KLABU KUFANYA MAZOEZI UK.24

MAONI, KATUNI UK.6



Mchuuzi wa nyama ya kuku akifanya biashara katika mazingira hatarishi kwa afya za wateja wake, kutokana na tope jingi katika soko la Msasani 'Maandazi Road', jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Agizo la Mbowe latikisa Chadema

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

MBUNGE wa Momba (Chadema), David Silinde, amemwandikia barua Mwenyekiti na Katibu Mkuu wa chama chake taifa, kujiuzulu nyadhifa zake zote.

Akizungumza na wanahabari katika viwanja vya Bunge, Silinde ambaye alianza kuingia bungeni juzi licha ya kuwapo agizo la Mwenyekiti wa chama hicho, Freeman Mbowe, kuwataka kujitenga ka siku 14 na kutofika eneo lolote la Bunge.

Alisema amepokea ujumbe Mnadhimu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Ester Bulaya, akimtaka kujiuzulu nafasi zake zote, na kwamba alifanya hivyo juzi.

Kupitia ujumbe wake wa Twiter aliandika:" Wabunge wa Chadema wamemtaka David Silinde ajiuzulu nafasi zake zote za uongozi kwa kushindwa kusimamia makubaliano ya chama. Kama Mnadhimu wa kambi ya upinzani naunga mkono, anapaswa kujiuzulu."

Mbunge huyo alisema juzi alijivua nafasi ya ukatibu wa wabunge na Msemaji wa kambi katika Wizara ya Viwanda, Biashara, ikiwa ni siku ya Wizara hiyo kuwasilisha makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2020/21.

"Watanzania wafahamu nipo hapa bungeni kwa udhamini wa vyama vyetu vya siasa, lakini waliotupigia kura ni wananchi, na mimi naongoza Jimbo la Momba kupitia Chadema," alisema na kuongeza:

"Kwa hiyo ikitokea siku Chadema wakininyima nafasi ya kugombea kupitia Jimbo la Momba, wananchi watanichagua kwa chama kingine ama Chadema wanaweza kunipa udhamini, na bado wananchi wakakataa nisirudi hapa bungeni."

Kwa mujibu wa Silinde, idhini ya mtu kufika bungeni ni wananchi na siyo chama cha siasa, chama cha siasa ni kama mdhamini tu.

"Nimekuja, kwa sasa kuna matatizo mengi ambayo yanatakiwa kutatuliwa, lile azimio la Mwenyekiti sio baya kwa sababu anataka sisi Wabunge tujilinde, lakini wananchi ambao tunaowaongoza wanaendelea kufa... binafsi sioni kama ina mantiki sana kwani tukijilinda sisi Wabunge baada ya siku 14 tunarudi hapa bungeni tunakutana na watu wale wale na Bunge ni lile lile," alisema.

Mbunge huyo alisema anatekeleza ahadi yake kwa wananchi kwa kuwa wakati anaomba kura, aliahidi kupambana hadi dakika ya mwisho, na ikiwezekana kufa, na siyo kukimbia.

# 13 wafa ajalini Pwani, Tanga

**Na Waandishi Wetu**

WATU wanane wamefariki dunia mkoani Pwani katika matukio mawili tofauti likiwamo la ajali iliyoua watu sita na wawili kuchomwa moto hadi kufa.

Vilevile, watu watano wamefariki dunia papo hapo na wengine wawili kujeruhiwa baada ya magari mawili ya mizigo kugongana uso kwa uso wilayani Korogwe mkoani Tanga.

Tukio la ajali ya kwanza lilitokea usiku wa kuamkia jana eneo la Vigwaza, Chalinze barabara kuu ya Morogoro na kusababisha vifo vya watu sita.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Wankyo Nyigesa, alithibitisha kuwapo kwa matukio hayo, akibainisha kuwa tukio la ajali lilihusisha gari lenye namba za usajili T299 AGE aina ya Toyota Prado, lililogongana na gari la mizigo lenye namba za usajili T469 DCP/T 996 BHH aina ya Scania lililokuwa limeegeshwa pembeni mwa barabara.

Kamanda Wankyo alisema, gari hiyo aina ya Prado ambalo dereva wake bado hajafahamika, lililigonga Scania lililokuwa likiendeshwa na Edger Mbilinyi (30), mkazi wa Njombe.

Alisema, watu waliofariki dunia wote ni wanaume na kati yao yupo mtoto anayekadiriwa kuwa na umri kati ya miaka 6-7.

Alisema majina yao hayajafahamika na majeruhi mmoja amefahamika kwa jina la Adinani Mresi (30), anayedaiwa kuwa askari wa JWTZ Ngerengere Morogoro aliyeumia sehemu mbalimbali za mwili wake.

Kamanda Wankyo alisema, chanzo cha ajali hiyo kinadaiwa kuwa ni dereva wa gari T 299 AGE, Toyota Prado kuendesha kwa mwendo kasi bila kuchukua tahadhari.

Wakati huo huo, Jeshi la Polisi linaendesha msako mkali kuwabaini walioshiriki katika tukio la kushambulia kwa matofali na marungu na kisha kiwachoma moto watu wawili wakiwatuhumu kuhusika na wizi wa pikipiki huko Msanga Zalala Wilaya ya Kisarawe.

Kamanda Wankyo alisema, tukio hilo lilitokea Mei 4, majira ya saa tatu usiku. Fortunatus Richard (20) na Omari Beyuu (20), wote wakazi wa Homboza waliuawa kwa kushambuliwa kwa matofali na marungu na kisha miili yao kuchomwa moto wakiwa kwenye pikipiki yao.

Aliwaonya wananchi wanaojichukulia sheria mkononi kuacha mara moja kwa kuwa wahalifu wote wanatakiwa kuripotiwa katika vituo vya polisi na si vinginevyo.

Ajali ya mkoani Tanga ilithibitisha na Kamanda wa Polisi mkoani huko, Blasius Chatanda, aliyesema tukio hilo lilitokea juzi majira ya saa 10 jioni katika eneo la Vigaeni mpakani mwa Kijiji cha Hale na Segera na kusabaisha vifo vya watu watano.

Chatanda alisema ajali hiyo ilihusisha gari lenye namba T 225 CRN, Scania lililokuwa likitokea upande wa Segera kuelekea mjini Tanga ambalo lilibeba mahindi na lingine lenye namba T 689 BEK, Fuso lililokuwa likitokea Tanga na kuelekea Upare likiwa na shehena ya simenti.

Aliwataja waliofariki dunia katika ajali hiyo kuwa ni Yusuf Salim ambaye alikuwa dereva wa Fuso na Athumani Mrisho aliyekuwa dereva wa Scania ambao wote walifariki papo hapo na wengine watatu ambao hawakutambulika majina yao kwa wakati huo.

***Imeandikwa na Julieth Mkireri (KIBAHA) na Hamida Kamchalla (TANGA)**

# Magonjwa yanayoua wabunge kutotajwa

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

BUNGE limesema kuwa halitatangaza ugonjwa wa mbunge yeyote kwa kuwa ni siri ya mgonjwa na hiari iko kwa familia yake kutangaza.

Akihitimisha kikao cha Bunge juzi jijini Dodoma, Naibu Spika, Tulia Akson, alitoa kauli hiyo baada ya kuwapo kwa hoja ya Mbunge wa Rombo, Joseph Selasini, aliyesema kuwa hakuna ushahidi kuwa kuna mbunge amekufa kwa corona.

Aprili 20, mwaka huu, Naibu Spika alilijulisha bunge kuwa mbunge mmoja (jina limehifadhiwa) amepata maambukizo ya corona na anaendelea na matibabu.

"Waheshimiwa wabunge sisi sote ni viongozi tunafahamu ugonjwa wa mtu ni siri yake yeye peke yake, akitaka sana yeye na daktari, sasa hatuwezi kufika mahali tukalazimishana kwamba mtu aseme ugonjwa wake ni nini ama mtu mwingine amsemee mtu mwingine kwamba amekufa na ugonjwa gani," alisema.

Alifafanua kuwa wale walioumwa Covid-19 wametangaza wao wenyewe na hakuna mahali serikali inasema nani amekufa na ugonjwa gani kwa sababu kila mtu ana ugonjwa wake na ugonjwa ni siri ya mtu.

"Kama ameamua kusema hilo ni suala lake kama hakusema mkakuta mauti imemchukua ameondoka nayo siri yake yeye na daktari, haimhusu mtu mwingine," alisema.

Kwa mujibu wa Naibu Spika huyo, hakuna mahali Bunge litafika kutangazia wabunge kuwa mtu amekufa na kifo fulani hilo halitowezekana na libaki hivyo.

"Nadhani tutakuwa tumefuata miongozo yote ambayo inawataka wenzetu kwenye eneo la afya kufanya hivyo nasi tusingetaka kuingia kwenye eneo hilo," alifafanua.

Wabunge waliofariki tangu kuanza kwa vikao vya Bunge ni Mbunge wa Newala Vijijini (CCM), Rashid Akibar, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Dk. Getrude Rwakatare, Mbunge wa Korogwe Vijijini (CCM), Stephen Ngonyani maarufu kama Profesa Majimarefu, Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Dk. Elly Macha, Mbunge wa Dimani (CCM), Hafidh Ally Tahir, Mbunge wa Songea Mjini (CCM), Leonidas Gama, Mbunge wa Buyungu, Kasuku Bilago, Mbunge wa Sumve (CCM), Richard Ndassa na Waziri wa Katiba na Sheria, Balozi Dk. Augustine Mahiga.

# Wachenjuaji dhahabu wapewa siku 30 kujisajili

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limetoa siku 30 kwa wachenjuaji wa dhahabu nchini kusajili miradi yao.

Limesema kwa kufanya hivyo, baraza watakuwa wametimiza hitaji la Sheria ya Hifadhi ya Mazingira ya 2004, na kwamba watakaoshindwa kufanya hivyo shughuli zao zitasimamisha, au kutozwa faini au kushtakiwa.

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alisema jana kuwa baraza linaamini ndani ya siku 30 litakuwa limekamilisha usajili kwa kuwa utafanyika kwa kutumia mtandao. Wenye miradi wanaweza kusajili moja kwa moja makao makuu ya baraza au katika ofisi zake za kanda katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Kigoma, Mbeya, Mtwara na Mwanza.

"Kwa mujibu wa sheria ya mazingira, miradi yote inatakiwa kuwa na cheti cha Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) au Cheti cha Ukaguzi wa Mazingira, hivyo tunawataka wawekezaji wote wanaojihusisha na miradi hiyo kusajili miradi yao ndani ya siku 30," alisema Dk. Gwamaka.

Dk. Gwamaka alisema kuendesha miradi bila kuwa na cheti cha TAM au cha Ukaguzi wa Mazingira ni kosa kisheria na hatua kali zinaweza kuchukuliwa ikiwa ni pamoja na kufungiwa kufanya shughuli hizo.

"NEMC tumekuwa tukichukua hatua za haraka katika kuhakikisha miradi ya maendeleo inafanyika bila kuleta athari hasi katika mazingira. Tunaamini ndani ya siku 30 tutakuwa tumefanikiwa kusajili miradi hiyo kwa kuwa inafanyika kwa njia ya mtandao kupitia ofisi zetu makao makuu au ofisi za kanda," alisema.

Alitoa wito kwa wenye miradi kuwatumia wataalamu elekezi ambao wamekidhi matakwa ya kisheria na wanatambuliwa na NEMC na baada ya siku 30 ukaguzi mkali utafanyika kuwabaini wasiotekeleza agizo hilo.



Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, akifafanua jambo kwa waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, wakati akitoa taarifa ya serikali kuvifuta vyama vya ushirika 3,348 nchini vilivyoshindwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria namba 6 ya mwaka 2013 ya vyama vya ushirika pamoja na vile ambavyo vilikuwa vyama hewa. Kulia ni Naibu wake, Omari Mgumba. **PICHA PAUL MABEJA**

# Serikali yafuta vyama vya ushirika 3,348

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imevifuta vyama vya ushirika 3,348 ambavyo vilikuwa havifanyi kazi, ama kutotekeleza majukumu yake ya msingi na vyama hewa.

Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, alitoa tangazo hilo jana jijini Dodoma, wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maendeleo ya vyama vya ushirika nchini.

Alisema uamuzi huo unatokana na kusudio la serikali alilotangaza Januri 5, mwaka huu, la kutaka kuvifuta vyama hivyo.

"Kwa mujibu wa kifungu cha 100 cha Sheria ya Vyama vya Ushirika Namba 6, ya mwaka 2013 na kanuni ya 26 ya kanuni za vyama vya ushirika za mwaka 2015, tulitoa notisi ya siku 90 ya kusudio la kuvifuta vyama 3,436 kutoka katika daftari (Rejista) la vyama vya ushirika," alisema Hasunga.

Alisema katika notisi hiyo ya siku 90, serikali ilitoa nafasi kwa mtu, chama au taasisi yoyote yenye mapingamizi kuhusu kufutwa kwa vyama hivyo vya ushirika vilivyoorodheshwa kuwasilisha kupitia ofisi za warajis wasaidizi wa mikoa.

"Notisi hiyo iliisha tarehe 17, Aprili mwaka huu na hivyo kuniwezesha kuvifuta vyama ambavyo havijajitokeza kupinga," alisema Hasunga.

Pia, alisema kabla ya muda wa kutoa mapingamizi kumalizika, serikali kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) ilipokea jumla ya mapingamizi 88, ambayo yalichambuliwa na kufikiwa uamuzi wake kwa kuzingatia maoni ya Warajis wasaidizi wa mikoa husika.

Alisema kutokana na hali hiyo serikali imejiridhisha na kukubaliana na mapingamizi hayo ya kutofutwa kwa vyama 88, na kuwa Warajis wasaidizi wa mikoa watawajibika kusimamia vyama hivyo vinaendeshwa kwa matakwa ya sheria.

"Hivyo basi ninatangaza kuvifuta rasmi vyama vya ushirika 3,348 ambavyo vingi ni hewa," alifafanua Hasunga.

Vile vile, alieleza kuwa mchanganuo wa vyama hivyo vilivyofutwa na idadi kwenye mabano kuwa ni Saccos (2,513), Amcos (229), Mifugo (77), vyama vya walaji (27), vyama vya huduma (70), vyama vya ufugaji nyuki (15), nyumba (9), madini (22), viwanda (79), uvuvi (32), umwagiliaji (31) na vinginevyo (244).

Alisema kuwa kufuatia kufutwa kwa vyama vya ushirika 3,348 kwa sasa Rejista ya vyama vya ushirika nchini itabaki na jumla ya vyama 8,611.

Waziri Hasunga, alisema kuwa utaratibu wa serikali kuvifuta vyama utakuwa endelevu kwa vile vitakavyo shindwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria.

"Natoa wito kwa wakulima au wanachama wanaovitumia vyama vya ushirika nchini kufungua akaunti benki ili mkulima kujihakikishia malipo yake, hii itakuwa mojawapo ya suluhu kwa udanganyifu unaofanywa na baadhi ya viongozi wa vyama vya ushirika wasio waaminifu," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Tume ya Ushirika nchini, Dk. Titus Kamani, alisema kitendo cha serikali kuvifuta vyama 3,348 inaonyesha nia yake ya kuimarisha ushirika kwa kuwa ndiyo jambo la msingi katika kujenga uchumi imara kwa wananchi wake.

# Wakili Dk. Lamwai afariki dunia

**Na Romana Mallya**

MWANASIASA na mwanasheria nguli, Dk. Masumbuko Lamwai, amefariki dunia jijini Dar es Salaam.

Taarifa za kifo chake zilithibitishwa jana na mdogo wa marehemu, Joseph Selasini ambaye ni Mbunge wa Rombo mkoani Kilimanjaro (Chadema).

Akizungumza na Nipashe, Selasini alisema kaka yake alizidiwa na kukimbizwa hospitali binafsi ya Rabininsia iliyoko Tegeta jijini Dar es Salaam, lakini baada ya kufikishwa huko, walishauriwa apelekwe Hospitali ya Lugalo au Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) na alifariki dunia usiku wa kuamkia jana wakiwa njiani kumwahisha hospitalini.

Kuhusu utaratibu wa mazishi, Selasini alisema utatolewa mara baada ya kikao kufanyika.

Alisema mwili wake umehifadhiwa Hospitali ya Jeshi Lugalo na msiba uko nyumbani kwa marehemu huko Kunduchi jijini.

Hadi anafariki dunia, Dk. Lamwai alikuwa Mkuu wa Kitengo cha Sheria katika Chuo Kikuu cha Tumaini Kampasi ya Dar es Salaam (Tudarco).

Aliwahi kuwa Mbunge wa Ubungo na baadaye Mbunge wa Kuteuliwa na Rais, Benjamin Mkapa.

Mwaka 1994, Dk. Lamwai aligombea udiwani wa Manzese, Jimbo la Ubungo na aliibuka mshindi akiwa kiongozi pekee wa upinzani mkoani Dar es Salaam na hakuishia hapo, akiwania nafasi ya Meya wa Jiji na kuambulia kura moja.

Katika uchaguzi mkuu wa mwaka 1995, Dk. Lamwai aligombea kiti cha ubunge wa Ubungo kupitia NCCR-Mageuzi na kushinda na kuwa mbunge wa kwanza wa upinzani jijini Dar es Salaam.

Mwaka 2000, Dk. Lamwai aliamua kujiunga na Chama Cha Mapinduzi (CCM) na kuachana rasmi na siasa za upinzani.

Mbali ya siasa, Dk. Lamwai alikuwa mwanasheria nguli na Mkufunzi Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na Chuo cha Tumaini.

RIPOTI MAALUM -3

# Hii ndiyo hatima ya korosho msimu huu

**Na Sanula Athanas,** ALIYEKUWA DODOMA

## Waziri afuatilia Sh. bilioni 124 'zilizopigwa' Ushirika

TOLEO la jana lilikuwa na ufafanuzi wa kina kuhusu hali ya akiba ya chakula nchini na zao la biashara la pamba. Waziri Japhet Hasunga, leo hii ana ufafanuzi wa kina kuhusu hatima ya korosho, zao lililopata msukosuko msimu uliopita.

Vilevile, ana maelezo ya kina kuhusu Sh. bilioni 124 zilizotoweka kiutatanishi kwenye vyama vya ushirika.

....... ....... ....... ....... .......



Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda (kushoto) akiteta jambo na Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, kwenye moja ya mashamba ya kiongozi huyo wa zamani wa serikali mkoani Dodoma mwezi uliopita. **PICHA: MAKTABA**

MWAKA wa fedha uliopita, serikali ilipanga bei elekezi ya Sh. 3,300 kwa kilo ya korosho na kuwataka wanunuzi wote kununua korosho za daraja la kwanza kwa bei hiyo.

Hatua hiyo ilisababisha wanunuzi wengi kugomea kununua zao hilo kwa maelezo kwamba bei elekezi hiyo ilikuwa kubwa na wasingepata faida wakati wa kuuza.

Baada ya mgomo huo, serikali iliamua kununua korosho zote zaidi za tani 200,000 kutoka kwa wakulima. Endelea na ufafanuzi wa maswali na majibu:

**SWALI: Wakati unateuliwa kuwa Waziri wa Kilimo, kulikuwa na tatizo katika soko la korosho inayozalishwa nchini. Uhai wa soko la korosho msimu huu ukoje na corona hii?**

**HASUNGA:** Ni kweli kabisa wakati ninateuliwa kulikuwa na tatizo la soko la korosho na limetusumbua sana mpaka sasa hatujamaliza kuwalipa wakulima. Mpaka sasa, wakulima bado wanatudai zaidi ya Sh. bilioni 20. Bado hatujamaliza kuwalipa.

Hii inatokana na udanganyifu uliojitokeza katika baadhi ya maeneo ambayo bado tunafanya uhakiki. Tukikamilisha, wakulima wote watalipwa hizo hela zao.

Tulichokifanya katika msimu uliofuata, ambao tumeusimamia mwaka huu na umeleta mafanikio makubwa, tuliwaruhusu soko binafsi wanunue moja kwa moja, lakini soko liwe la wazi.

Tuliamua sasa sanduku (la zabuni) litawekwa saa mbili kamili asubuhi na litafungwa saa 10 jioni, litafunguliwa katika eneo la wazi na watu wote watashuhudia katika kufungua na tutamwona nani ameahidi nini na amefanya nini na hicho alichoahidi. Kama ameshinda, huyo ndiye atatangazwa mshindi na kupatiwa zile korosho.

Hii itasaidia sana kuondokana na dosari zilizokuwapo miaka ya nyuma na udanganyifu na rushwa zilizokuwapo zitafutwa. Kwa hiyo, kwa kiwango hiki tunaweza kufanikiwa sana.

Lakini, sasa hivi katika kipindi hiki cha corona, tuna imani hii minada ambayo bado tunaiendesha vizuri sana kwa mwaka huu, huenda isifanikiwe kwa sababu watu wengi watashindwa kusafirisha na kuja nchini kushiriki minada.

Tunachokusudia kufanya, ni kuuza kwa TMX (kwa mtandao). Tunauza kwa njia ya mtandao, wanunuzi watakaa huko huko waliko, lakini watakuwa na uwezo wa kutoa ofa zao na kupata korosho zao kwa kadri watakavyoona inafaa. Tuna imani katika hili, itatusaidia.

La pili, nimeagiza Bodi ya Korosho iende na vyombo vya ushirika wakatembelee masoko, wawasiliane na wanunuzi wakubwa, waingie katika mikataba ya moja kwa moja ya kuuziana bidhaa.

Yaani kwa sasa mtu akileta bei ambayo tunaiona kwamba ni nzuri na 'reasonable' (inayokubalika) na iko kwenye kiwango cha soko la dunia, basi tunaingia naye mkataba wa moja kwa moja. Kinachobaki sasa ni kwenda kusafirisha tu mzigo na kumpelekea.

Lazima tuingie mikataba ya moja kwa moja, badala ya kutegemea kuja kuanzisha minada maana isipofanikiwa, inakuja kuwa dosari. Kwa hiyo, tunafikiri utaratibu huu unaweza kutusaidia sana.

Na tumeagiza pia balozi zetu zote zitafute wanunuzi huko ili tuzungumze nao, tuingie mikataba ya mauziano ya korosho. Hii itakuwa ni njia ambayo inaweza ikasaidia.

Jambo la mwisho, tumezungumza pia na wawekezaji mbalimbali kutoka Marekani na maeneo mengine, nchi za Scandinavia (Denmark, Norway na Sweden), wanataka waje wajenge viwanda vya kuongeza thamani.

Tukiongeza thamani, tukabangua korosho hapa nchini, soko la korosho nchini litakuwa vizuri. Kwa mwaka huu, hatuwezi kusema tutabangua zote kwa sababu hata viwanda vyenyewe ambavyo vipo, viko 30, vingine havijajengwa, lakini lazima tutafanya hicho kitu kizuri.

**SWALI: Uhai mpya wa ushirika ulioibuliwa na Rais John Magufuli na viwanda vyake, unakusaidiaje?**

**HASUNGA:** Kwa kweli umetusaidia sana. Maelekezo ya Mheshimiwa Rais kwamba 'tunataka ushirika ambapo serikali itaweka mkono, ushirika ambao utasimamiwa ipasavyo, ambao utakuwa ni tumaini la wakulima wengi' na Watanzania kwa ujumla', yamefanikiwa kwa kiwango kikubwa na yameleta ari mpya.

Wakulima hawana chombo chochote cha kuwaunganisha. Ni kupitia ushirika ndiyo unaweza ukawaunganisha wakawa kitu kimoja, wakazungumza kwa sauti moja, wakajadiliana bei ya mazao yao kwa sauti moja. Ndiyo ushirika ambao tunautaka.

Ushirika ambao unaweza ukamhudumia mkulima, ushirika ambao utajua mkulima wake anahitaji pembejeo gani, anahitaji mbegu gani na atapataje kipindi ambacho hana hela, ushirika ambao utaweza kuwakopesha wanachama wake. Ndiyo ushirika ambao tunautaka.

Kikubwa ambacho kilikuwa kinafanyika kwenye uendeshaji wa ushirika, ni ubadhirifu mkubwa kwenye mali za ushirika na fedha za ushirika.

Hatua gani ambazo tumezichukua? Utaona wizara tumeanza kuchukua hatua kutokana na maagizo ya Mheshimiwa Rais. Tumesimamia ukaguzi wa vyama vya ushirika na ripoti ikatolewa. Yale yaliyoonekana ni upungufu, tumeanza kuwachukulia hatua.

Na kwa kujua kuna mamlaka zile za kuwafikisha watu mahakamani, nilichukua zile ripoti, nikaikabidhi Takukuru (Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa) ili wawakamate wale na kuwapeleka mahakamani na wewe umeona jinsi Takukuru walivyopambana katika hilo na sisi tunawashukuru sana.

Katika maelekezo yangu, ilionekana kuna karibu Sh. bilioni 124 zilikuwa zimeibwa kipindi kile na vyama vya ushirika. Kwa hiyo, bado ninalifanyia kazi.

Mpaka sasa, wamehakiki Sh. bilioni 68, wanaendelea na uhakiki ili tubaini hasa ni kiasi gani cha fedha ambacho kimeibwa na vyama vya ushirika na wale walioiba, wachukuliwe hatua na wazirejeshe hizo fedha.

Tuna imani kwa kufanya hivyo, kwanza itakuwa ni fundisho kwa vyana vya ushirika, wataacha kujishirikisha na wizi. La pili, wananchi watakuwa sasa na imani na vyama vya ushirika na kila kiongozi atakayekuwapo pale, atakuwa anawahudumia wananchi moja kwa moja.

Tatu, watu hawatataka tena kudhalilika kama walivyodhalilika mwaka huu. Maana wale watu tukiwakuta ni wezi, tunakamata mali zao, tunakamata nyumba zao, tunawafikisha mahakamani, wanashtakiwa kwa Sheria ya Uhujumu Uchumi. Hiyo sasa imetuletea ari mpya na mambo yanakwenda vizuri.

Pia, tunapitia upya Sheria ya Ushirika ili kurekebisha dosari mbalimbali zilizojitokeza zilizotokana na mfumo wa sheria, na kuangalia sifa za viongozi, ili kiongozi anayesimamia ushirika awe somo au taaluma fulani. Tunataka hao ndiyo wasimamie ushirika, ili ushirika uwe na manufaa makubwa kwa wananchi wote.

- **JE, MABWANA SHAMBA NA WATAALUMA WA FANI HIYO NA SUALA LA MABORESHO LINA NAFASI GANI KATIKA KUINUA KILIMO? FUATILIA KESHO.**

HABARI KITAIFA

# Mazungumzo kigogo wa Jaruma, DPP, TRA yaendelea

**Na Hellen Mwango**

UPANDE wa utetezi katika kesi inayomkabili Mkurugenzi wa Kampuni ya Jaruma General Supplies Ltd, Lucas Mallya na wenzake watano, umedai mahakamani kwamba umemwandikia barua Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini (DPP) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) bado wanaendelea na majadiliano.

Mallya na wenzake wanakabiliwa na mashtaka 23 ya uhujumu uchumi ikiwamo kukwepa kodi ya vileo, kuisababishia serikali hasara na kutakatisha zaidi ya Sh. bilioni 31.48.

Kesi hiyo ilipangwa kutajwa jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mfawidhi, Godfrey Issaya.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kuwa kesi hiyo imepangwa kwa ajili ya kutajwa upelelezi wake bado haujakamilika aliomba tarehe nyingine ya kitajwa.

Wakili wa utetezi, Hudson Ndusyepo alidai kuwa wameandika barua kwenda kwa DPP na TRA ya kukiri makosa na bado wanaendelea na mazungumzo.

Hakimu Isaya alisema kesi hiyo itatajwa Mei 20, mwaka huu. Mallya na wenzake wote wanadaiwa kusababisha hasara jumla Sh. 31,489,529,153.07.

Wankyo aliwataja washtakiwa kuwa ni, Happy Mwamugunda, Prochesi Shayo, Geofrey Urio, Mhasibu Tunsubilege Mateni na Mkaguzi wa hesabu, Nelson Kahangwa.

Katika shtaka la kwanza washtakiwa wote wanadaiwa kati ya Januari 2015 na Januari 7, 2020 jijini Dar es Salaam kwa pamoja waliongoza genge la uhalifu kwa nia ya kupata faida.

Ilidaiwa katika shtaka la pili mpaka la saba linamkabili Mallya anadaiwa Juni 3, 2019, jijini Dar es Salaam alighushi kutengeneza stempu ya ushuru akionyesha imetengenezwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) wakati si kweli.

Ilidaiwa kuwa alitoa nyaraka hiyo ya kughushi TRA akionyesha ni halali wakati akijua si kweli na katika shtaka lingine inadaiwa Januari 7, mwaka huu, Chang'ombe A, Temeke, jijini Dar ea Salaam alikutwa na lora 93 za stempu zenye thamani ya Sh. 80,516,000 alizochapisha bila kibali cha Kamishna wa Mapato.

# Waziri aanika mikakati viwanda kukabili corona

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

WIZARA ya Viwanda na Biashara, imesema jumla ya viwanda na taasisi 12 nchini, vinatengeneza vifaa tiba kwa ajili ya kukabiliana na homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya corona.

Akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka ujao wa fedha, Waziri Innocent Bashungwa alisema vifaa hivyo ni barakoa, vitakasa mikono na mavazi maalumu kwa watoa huduma za afya.

Alisema viwanda vidogo 55 vya nguo na mavazi pia vimeunga mkono kwa kuanza kutengeneza barakoa kwa kutumia malighafi ya kitambaa, na kwamba tayari kuna viwanda 40 vya kutengeneza vitakasa mikono vilivyosajiliwa hadi sasa.

Alisema katika kukabiliana na corona Machi mwaka huu, wizara yake ilikutana na wazalishaji wa malighafi ya kutengeneza vitakasa mikono (ethanol) na wazalishaji wa bidhaa hizo, lengo likiwa kujadiliana na wenye viwanda na wadau wengine namna ya kufanikisha utengenezaji na upatikanaji wa vifaa kinga vya kuzuia usambaaji wa ugonjwa huo.

"Viwanda hivyo vimeitikia wito wa kuunga mkono serikali katika vita dhidi ya ugonjwa huo. Kwa mfano, Kiwanda cha Kilombero kinachomilikiwa kwa ubia na serikali, kilichangia jumla ya lita 30,000 za ethanol kwa ajili ya kutengeneza vitakasa mikono na Wizara ya Afya ilipewa lita 20,000 na kiasi kilichobaki zilipewa taasisi za Sido na Trido.

"Mwitikio huo umehamasisha uwekezaji katika viwanda vya kutengeneza barakoa, vitakasa mikono, sabuni za kunawa mikono na ili kuongeza upatikanaji wa bidhaa hizo," alisema.

Kwa mujibu wa waziri huyo, Trido ilitengeneza kitakasa mikono ambacho tayari kinatumika kwa jamii kwa ajili ya kujikinga na kuzuia kuenea kwa maambukizo ya corona. "Mpaka sasa, Trido imetengeneza lita 202 za vitakasa mikono na kuwafikia watu mbalimbali kwa ajili ya matumizi.

"Wizara inaendelea na kazi ya ufanyaji tathmini ya mahitaji ya vitakasa mikono nchini kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Mkemia Mkuu wa Serikali, wazalishaji wa ethanol na Mamlaka ya Chakula na Vifaa Tiba (TMDA)," alisema.

Waziri Bashungwa alisema kupatikana kwa takwimu halisi kutasaidia serikali kufanya uamuzi wa haraka hususan ya kuagiza ethanol ambayo ni malighafi muhimu katika kutengenezea vitakasa mikono.

**AONYA WAFANYABIASHARA**

Waziri huyo pia aliwaonya wafanyabiashara wanaotumia mazingira ya ugonjwa huo kama fursa ya kujinufaisha badala ya kuunga mkono juhudi za serikali katika kupambana na janga hilo.

"Nawasihi wajielekeze katika kulinda afya za wananchi wetu kwani serikali haitasita kuchukua hatua kali za kisheria kwa wote watakaobainika kujihusisha na vitendo vya aina hiyo," alionya.



Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam, wakipita jirani na rundo la takataka zilizotelekezwa kando ya barabara katika eneo la Tandale Sokoni, jijini humo jana, na kusababisha usumbufu kwa waenda kwa miguu na wafanyabiashara wenyewe. **PICHA: MIRAJI MSALA**.

# Athari za corona mazao yanayosafirishwa nje zatajwa

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

WIZARA ya Viwanda na Biashara, imeeleza athari za kiuchumi zilizosababishwa na janga la corona katika mazao ya biashara yanayosafirishwa kwenda nje.

Akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2020/21, Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, alisema biashara hizo hutegemea usafiri wa anga kuingia katika nchi mbalimbali ambao kwa sasa haupo, ikiwa ni jitihada za kujikinga na corona.

Alisema athari kubwa zaidi ni kwenye mazao kwa kuwa Tanzania soko lake liko katika nchi za kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), Jumuiya ya Ulaya (EU), Asia, China, India na Japan na AGOA, na kwamba bidhaa inazouzwa kwa wingi ni almasi, dhahabu, chai, kahawa, maua na viungo.

Bashungwa alisema baadhi ya mazao ya kimkakati yakiwamo pamba, korosho na kokoa bei zake zimeshuka.

"Katika kipindi cha Februari na Machi 2020, bei ya pamba duniani imeshuka kwa asilimia 12, kakao kwa asilimia 22 na kahawa kwa asilimia 5 (Arabika) na asilimia 3.5 (Robusta) kutokana na kufungwa kwa maduka nchini China, Ulaya na Marekani kutokana na zuio la kutotoka nje," alisema.

Alitolea mfano Kampuni ya Starbucks kufunga maduka 2,150 kati ya 4,300 nchini China, na kwamba mauzo ya mazao na bidhaa za kilimo yameshuka.

Aidha, alisema kiwango cha ununuzi wa kakao kilishuka kutoka tani 116,440 Februari 2020 hadi kufikia tani 38,354 mwezi Machi 2020 ikiwa ni sawa na asilimia 67.1.

Kwa upande wa wazalishaji wa mazao ya mboga, matunda, maua na viungo kwa miaka mingi wanategemea soko la nje hasa Ulaya, Marekani na Asia.

"Kutokana na mlipuko wa ugojwa huo na kufungwa kwa mipaka, kumeathiri biashara hiyo ambayo mazao yake yanaharibika kwa wepesi," alisema Waziri Bashungwa.

Alifafanua jinsi biashara ya mazao hayo iliyoathirika kuwa ni mauzo ya mazao ya mboga na matunda nchini kumeshuka kwa asilimia 50.

"Hali hiyo imesababishwa na kushuka kwa mahitaji ya bidhaa hizo hususan katika soko la nje, na kupungua kwa safari za ndege. mfano, Shirika la KLM limepunguza safari zake kutoka safari saba kwa wiki hadi tatu," alisema na kuongeza:

"Uhitaji wa mazao hayo katika masoko ya ndani ni mdogo na kukosa masoko mbadala wa kupeleka bidhaa zao zaidi ya kuendelea kuzihifadhi kwa muda mfupi na baadaye kuziteketeza kabisa."

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Si wakati kuwachekea wanaokataa barakoa

**SUALA** la kuvaa barakoa kwenye maeneo ya umma na sehemu zenye mikusanyiko mikubwa hasa maeneo ya ibada, sokoni, vituo vya mabasi na ndani ya vyombo vya umma si wakati wa kulichukulia kuwa ni jambo la hiari au mzaha.

Tunasema haya kwa sababu watu wanapuuza na kuchukulia uvaaji wa barakoa kama utani.

Wanaokataa kuvaa kila mmoja ana maelezo yake ya kujifariji wapo wanaosema hazina viwango, zinawalinda watu wengine hazimlindi mvaaji na madai ya kushindwa kupumua.

Kwa ujumla kila mmoja huja na utetezi wake wakihoji kuna viwango gani kwenye barakoa za vitenge? Tena wapo wanaotilia mashaka zile zinazotumiwa kwenye upasuaji hospitalini.

Katika maelezo yanayotolewa na wataalamu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), barakoa huepusha watu kuwaambukiza wenzao corona wakati wa kuongea, kupiga chafya, miayu na kukohoa. Inazuia mate na maji maji kutoka kinywani au puani kwa mtu anayezungumza au kupiga miayu kwenda kwa wengine.

Matumizi ya kinga hii ni muhimu, mathalani, mwaka 1918 kulizuka mafua hatari yaliyojulikana kama Spanish influenza pandemic na mwokozi akawa ni barakoa na kila mmoja alitakiwa kuvaa.

Licha ya kwamba hakuna sheria wala adhabu, lakini nilazima sasa wananchi wahimizwe kuvaa barakoa na ikibidi mabwana afya watembelee maeneo yenye mikusanyiko mikubwa kama kwa mama na babalishe, vibanda vya chips, vituo vya mabasi, ndani ya magari ya umma na kwenye maduka makubwa ya vifaa na bidhaa zinazonunuliwa kila wakati.

Kwa mujibu wa taarifa za mitandao, mafua ya Spanish yaliua mamilioni ya watu na kutumia barakoa ilikuwa njia mojawapo kubwa na ya muhimu ya kupunguza kusambaa maradhi hayo.

Kutoka na kuibuka corona, mataifa mengi yametunga sheria ya kuvaa kinga hiyo na nchi kama Ujerumani, Austria na Poland zinatajwa.

Kwa hiyo tunawaomba watu wavae kinga hizo. Si jambo la kupuuza tena ni muhimu pamoja na kuvaa wasikaribiane wahakikishe wanasimama umbali wa mita mbili kuepusha kusambaa virusi.

Tunaishauri serikali kuwatumia maofisa wa afya, mazingira, vyama vya wenye magari na polisi kufuatilia na kuhimiza uvaaji wa barakoa na kuwaonya watu wasipuuze maelekezo hayo.

Aidha, ni wakati wa kuwatumia makondakta na madereva kuwahimiza watu kuvaa barakoa kabla ya kupanda kwenye magari na pia kunawa mikono yao.

Kama ambavyo huwezi kuingia chumba cha daktari hospitalini bila kujikinga, ni lazima sasa watu wasiruhusisiwe kuingia sokoni, kwenye ibada, kwenye usafiri wa umma bila barakoa.

Lakini pia serikali iwahamasishe wazalishaji wa barakoa zenye viwango na kuweka maduka maeneo yenye watu wengi hasa stendi, sokoni na maeneo ya biashara zinazovuta watu wengi.

Pamoja na kuhimiza uvaa sahihi wa barakoa, ni wakati pia wa kuwakumbusha watu kuhusu umuhimu wa kutengeneza na kuuza barakoa kwa viwango kwa kuwapa muongozo.

Kwa mfano kuna madai kuwa wapo wanauza barakoa barabarani zimetundikwa na kuchafuliwa na vumbi, lakini kuna maelezo kuwa wateja wanazishika shika na kuzijaribisha na kusababisha uwezekano wa kusambaza maradhi.

Tunaishauri serikali kutoa muongozo ili kukomesha tatizo. Wizara ya Afya itoe maelekezo yatakayosimamiwa na halmashauri ili kuwalinda Watanzania na hatari zote na maambukizi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Jenifer Julius

# Uwe mwanzo wa kufunza watoto kujisomea vitabu

**LIKIZO** ya kujihadhari na corona kwa wanafunzi wote wa Tanzania imedhihirisha kuwa kuna ulazima wa kujifunza na kufundishwa kusoma vitabu badala ya kuendelea kuamini kuwa kusoma na kupenda vitabu ni kitu kinachoendana na mapenzi 'hobi'.

Ni wazi kuwa kama wanafunzi wetu hasa wa sekondari na vyuo mbalimbali wangekuwa na mazoea ya kusoma vitabu msimu huu wa livu ya tahadhari usingekuwa wa hasara kwao. Kwani wangeutumia kusoma vitabu vya aina mbalimbali na hata kujibu mitihani kwa njia ya mtandao.

Lakini kukosa mazoea ya kujisomea vitabu kumeonyesha jinsi kulivyo na athari kubwa katika jamii. Kwa wanafunzi hawa imewasababishia kukosa kufahamu mambo kwani wameshindwa kutumia muda huo kuchimba.

Ni wazi kuwa kutosoma kunasababisha kufeli mitihani kutokana na kuwa wavivu kujisomea ili kuongeza maarifa na wakati mwingine wengine wamepata alama ndogo kwenye mitihani hasa vyuo vikuu kutokana na kushindwa kujenga hoja za kuwashawishi wahadhiri kwa mifano mingi zaidi ambayo angewapatia alama nyingi mambo ambayo wangeyapata kwenye vitabu na makala mbalimbali.

Wanafunzi wengi hufeli somo la Fasihi kutokana na uvivu wa kusoma vitabu husika na kuvielewa, matokeo yake humeza vitini ambavyo vimefanyiwa uchambuzi wa vitabu hivyo, hali inayosababisha kutojenga hoja zenye kuwashawishi wasahihishaji ambazo ingekuwa rahisi kwao kama wangesoma vitabu na kuvielewa.

Hata katika muktadha mwingine kama vile kanisani, kwenye warsha na semina mbalimbali ,watu wamekuwa wategemezi wa kusikiliza wenzao tu na sio kujisomea wenyewe ili kuelewa zaidi, mfano kanisani mchungaji anaweza kufundisha na kutoa mistari katika Biblia ili watu wakasome na kujifunza zaidi ,wengi hawafanyi hivyo kwa kuona uvivu hivyo kubaki na uelewa kidogo.

Kutopenda kusoma kuna athari nyingi mathalani, ofisini kuna ambao wamesaini mikataba ya kazi inayowaonea kutokana na kutokuwa na mazoea ya kusoma kilichomo. Wanapokuja kushtuka baada ya kuona athari za mkataba waliyosaini tayari muda umeshakwenda na hawana la kufanya.

Ni ukweli kuwa kama ambavyo jamii yetu ilivyokosa ari ya kujisomea ndivyo na watoto wanavyokosa mwamko na ari ya kusoma, hivyo likizo ya corona itamalizika kwa wengi kubakia mbumbumbu licha ya kwamba wangeweza kufanya jambo la kujiongeza kitaaluma.

Usemi kuwa 'kuna nguvu kubwa katika kujisomea ' unamaana pana kwamba kupitia vitabu na majarida mtu anaweza kujifunza vitu mbalimbali kushinda hata vile ambavyo angekwenda shuleni. Inamaanisha kusoma vitabu kunampa msomaji elimu kubwa hata bila mwalimu. Kwa kifupi mtu anaweza kujitibu bila hata kwenda hospitali, mfano matatizo ya kisaikolojia, vipo vitabu mbalimbali vinavyoelezea jinsi ya kupambana na matatizo ya kisaikolojia kwa rika zote.

Katika kujisomea mtu anaweza kujifunza jinsi ya kukabiliana matatizo na vishawishi, mfano unaweza kukutana na safari za maisha za waandishi mbalimbali na jinsi walivyokabiliana na vishawishi, changamoto na shida nyingi lakini wakazivuka.

Mfano, kitabu cha I will, I must, I can kilichoandikwa na Dk. Reginald Mengi ,kinafundisha vijana na watu wote kusimamia ndoto zao na kuhakikisha zinafanikiwa na kuwafikisha pale wanapotaka ,wakikabiliana na changamoto zinazoambatana nao bila kuchoka.

Katika jamii yetu kuna tofauti kubwa ya kifikra na kimtazamo kati ya mtu mwenye utamaduni wa kujisomea vitabu na majarida na yule asiyekuwa na utamaduni huo.

Mwenye kusoma vitabu anajenga hoja nzito yenye mifano hai kwa kuwa anajua vitu vingi na hashindwi mambo. Lakini yule ambaye si wa vitabu utamsikia akiongea maneno yale yale kuwa kenge anaweza kufyoanza ubongo wa binadamu.

Kwa hiyo kinachotokea wakati huu kiwe funzo kuwa tunatakiwa kuanzisha masomo na mitihani ya kusoma vitabu. Taasisi za elimu zianze kufikiria jinsia ya kuwafundisha watoto wetu shuleni na vyuoni kusoma vitabu.

Kwa walioko likizo hawajachelewa hebu watumie muda huu kujifunza na kujizatiti kusoma vitabu hata kama hawajazoea.



Katibu wa Afya Mkoa wa Shinyanga, William Mambo, akitoa elimu kwa wahudumu wa afya wa wilaya za Kishapu na Shinyanga, kuhusu namna ya kutoa matibabu kwa wagonjwa wenye maambukizo ya virusi vya corona, katika semina mkoani humo juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**.

# Waziri: Kuifunga Dar zinahitajika tril. 2.5/-

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Mwigulu Nchemba, amesema ili kulifunga jiji la Dar es Salaam, zinahitajika zaidi ya Sh. trilioni 2.5 kwa mwezi kulipa watu.

Aidha, kama na majiji mengine yakifungwa zitahitajika Sh. Trilioni tano, fedha ambazo Serikali haina.

Akichangia mara ya kwanza baada ya kuteuliwa kuwa Waziri katika hotuba ya makadirio ya Wizara ya Viwanda na Biashara, alisema ni vigumu kwa Tanzania kuiga kila kilichofaywa na nchi nyingine kwa kuwa hali za wananchi wa Tanzania inajulikana.

"Wapo wanaosema Dar es Salaam ifungwe na watu walipwe, kazi zote zikisimama na kukakosekana kinachokusanywa na hatujui janga litaisha lini kwani huenda tukaishi nalo," alisema.

"Akiba iliyopo ukasema itawalipa kufunga jiji moja unahitaji si chini ya Sh. Trilioni 2.5 kwa mwezi kuwalipa watu, ukiweka na majiji mengine utahitaji Sh. trilioni 5 kwa mwezi kulipa," alisema.

Kwa mujibu wa Nchemba, kusema kwamba serikali inalinda uchumi kuliko maisha ya watu si kweli kwa kuwa wapo watu ambao hawana akiba, kile wanachozungusha ndicho wanachotumia, kulipa watu wasio na kazi ni jambo ambalo haliwezekani.

"Tuhakikishe tunajihami bila kutengeneza janga jingine...huwezi kushughulikia janga kwa kutengeneza janga jingine, tunaona nchi nyingine watu wamekufa kutokana na kutengeneza majanga ya kujitakia," alisema.

Mbunge wa Viti Maalum (CUF), Zainabu Mndolwa, aliitaka Serikali kuangalia uwezekano wa kuwaondolea kodi Watanzania ambao wanashindwa kufanyakazi kutokana na janga la corona.

"Itakapofika mwisho mwa mwaka endapo hawatalipa kodi walizokadiriwa mwanzoni mwa mwaka watatozwa faini. Naiomba Serikali ichukue hili na kuwasaidia wafanyabiashara wa Dar es Salaam," alisema.

Mbunge wa Geita Vijijini, Joseph Musukuma, aliiomba Serikali kuzungumza na nchi za Rwanda na Uganda kwa kuwa Watanzania wananyanyasika kuingia, lakini wao wanataka kuingia nchini.

"Inaonekana sisi ndiyo tunaongoza kuwa na corona dunia nzima, wao kuja Tanzania hakuna mashatri, na ndiyo maana Watanzania wanachukua hatua mkononi. Tunaomba diplomasia na Wizara ya Viwanda na Biashara kuangalia suala hili.'

Alisema magari ya Tanzania hayaruhusiwi kwenda kwenye hizo nchi, na wao wanakuja nchini kukaa mwezi mmoja kusubiria makontena kunekana ni jambo la kawaida.

# Corona yazuia sherehe za mavuno

**Na Happy Severine,** SIMIYU

WAKATI maandalizi ya kuanza msimu wa sherehe za mavuno mkoani Simiyu yakiendelea kwa mujibu wa utamaduni wa kabila la Wasukuma kila mwaka, serikali imezipiga marufuku kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Sherehe hizo ambazo hujulikana kama 'Mbina' hufanyika kila mwaka kwa kukutanisha makundi mbalimbali ya watu, ambao ushindanisha tamaduni za kabila la Wasukuma katika pande mbili za Wagika na Wagalu.

Kuwapo kwa sherehe hizo huashilia uwapo wa mavuno makubwa ya chakula, hivyo watu hutakiwa kusherehekea mavuno hayo na kufurahia kwa kuimba na kucheza ngoma za Kisukuma.

Wakati viongozi wa sherehe hizo wakiwa kwenye maandalizi Mei kila mwaka, serikali imewataka waandaaji kusitisha mpaka itakapotangazwa tena.

Mkuu wa Wilaya ya Bariadi mkoani Simiyu, Festo Kiswaga, alisitisha sherehe hizo jana, baada ya kupokea vifaa kwa ajili ya watoa huduma vilivyotolewa na mfanyabiashara, Henry Mchunga, na kusema kuwa mwaka huu sherehe hizo hazitakuwapo.

Kiswaga alimwagiza Mkuu wa Polisi mkoani humo kuhakikisha anatoa maelekezo kwa kila polisi kata pamoja na watendaji wa kata na vijiji, wahakikishe sherehe hizo hazifanyiki kwenye maeneo yao.

"Ikitokea kiongozi yeyote ameandaa sherehe hizo na zikafanyika, hatua kali zitachukuliwa dhidi yake...hata mtendaji wa kijiji au kata atachukuliwa hatua, serikali kwa sasa imepiga marufuku sherehe zozote kutokana na ugonjwa wa corona," alisema .


ewura

Energy and Water Utilities Regulatory Authority

ISO 9001:2015 Certified

MAKAO MAKUU

Ghorofa ya 4, Jengo la PSSSF, Barabara ya Makole

S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania

Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005

Barua pepe: info@ewura.go.tz Tovuti: http://www.ewura.go.tz

*Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ni Taasisi ya udhibiti wa huduma za sekta nne mchanganyiko inayojitegemea iliyoundwa na Sheria ya EWURA Sura Namba 414 ya Sheria za Tanzania. Shughuli kuu za Mamlaka ni pamoja na kudhibiti sekta za Nishati na Maji kwa Tanzania Bara. EWURA inawajibu wa kuzidhibiti sekta hizi kiufundi na kiuchumi. Mamlaka ina wajibu wa kudhibiti shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ndogo ya Mafuta na Gesi Asili. Pia Mamlaka inadhibiti Umeme na Maji Safi na Usafi wa Mazingira kwa kuhakikisha huduma zinazodhibitiwa zinapatikana kwa viwango vya ubora wa kutosha; kwa bei halisi; salama na kwa uhakika; na kwamba watoa huduma wanapata faida ya halali na stahiki kwenye vitega uchumi vyao.*

Sheria ya Mafuta Na. 21 ya mwaka 2015 inaipa nguvu EWURA, kusimamia shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli. Kifungu cha 131 (1) cha sheria hiyo kinawataka wote wanaojihusisha na sekta tajwa kuwa na leseni iliyotolewa na EWURA.

Kutokana na kifungu cha 19(4) cha Sheria ya EWURA, Sura Namba 414 ya Sheria za Tanzania, taarifa inatolewa kwa umma kwamba, wafuatao wameomba leseni kujihusisha na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli.

| S/No | Jina la Mwombaji | Eneo | Jina la Mkurugenzi/Uraia | Aina ya Leseni |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Tully Hallan Musyani S.L.P 2099 Mbeya | Eneo la Ilomba, Mbeya Mjini, Wilaya ya Mbeya, Mkoa wa Mbeya | Tully Hallan Musyani (Mtanzania) | Leseni ya Usambazaji Gesi ya Majumbani (LPG) |
| 2. | Alutz Company Limited S.L.P 876 Songea | Eneo la Jengo la Hanga, Manispaa ya Songea, Mkoa wa Ruvuma | Hainess William Nanyaro (Mtanzania) | Leseni ya Usambazaji Gesi ya Majumbani (LPG) |
| 3. | Hamwi Co. Ltd - Kimea Filling Station S.L.P 271 Muleba | Kijiji cha Hamatojo Mtaa wa Kimea Kata ya Kasharunga Wilaya ya Muleba Mkoa wa Kagera | Haningi Bahiganaki Stephano (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha mafuta |
| 4. | Ratel Trading & General Supplies S.L.P 55194 Mwanza | Eneo la Igoma Wilaya ya Ilemela Mkoa wa Mwanza | Geofrey Sabuni (Mtanzania) | Leseni ya usambazaji wa Gesi ya LPG |
| 5. | D.S Traders Company Limited S.L.P 47 Tarime | Kiwanja Na. 10 Kitalu 'B' Eneo la Sabasaba Wilaya ya Tarime Mkoa wa Mara | Simon Kiles Samwel (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha mafuta |
| 6. | Jeremiah Peter Mwaikatale S.L.P 22488 Dar es salaam | Eneo la Kibada, Wilaya ya Kigamboni, Mkoa wa Dar es salaam | Jeremiah Peter Mwaikatale (Mtanzania) | Leseni ya usambazaji wa Gesi ya LPG |
| 7. | Delta Africa Limited S.L.P 80496 Dar es salaam | Kiwanja Na.77, Eneo la Kinondoni,Wilaya ya Kinondoni, Mkoa wa Dar es salaam | Araz Mohammad (Mtanzania) | Leseni ya usambazaji wa Gesi ya LPG |
| 8. | Lodhia Steel Industries Ltd S.L.P 75778 Dar es salaam | Kiwanja Na.6/3, Kitalu "B", Kisemvule, Wilaya ya Mkuranga, Mkoa wa Pwani | Arun Lodhia (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta kwa matumizi binafsi |
| 9. | Saint Parts Co. Ltd S.L.P 77906 Dar es salaam | Eneo la Shaurimoyo, wilaya ya Ilala, Mkoa wa Dar es salaam | Koji Muroya (Raia wa Japan) | Leseni ya usambazaji vilainishi |
| 10. | Lucky Space Investment Limited S.L.P 63014 Dar es salaam | Kiwanja Na. 8, Eneo la mivinjeni – Kurasini, Wilaya ya Temeke, Mkoa wa Dar es salaam | Neema S. Toziri (Mtanzania) | Leseni ya jumla ya vilainishi |
| 11. | Mbuyuni Filling Station S.L.P 41 Ruangwa | Kijiji cha Nandagala, Wilaya ya Ruangwa, Mkoa wa Lindi | Bakari Mohamed Amanzi (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 12. | Chambo Oil Filling Station S.L.P 16126 Dar es salaam | Eneo la Sungaji, Wilaya ya Mvomero, Mkoa wa Morogoro | Hassan Hezron Kibona (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 13. | Lake Oil Sinza S.L.P 5055 Dar es salaam | Kiwanja.Na.5, Kitalu "A", Eneo la Sinza Makaburini, Wilaya Ubungo, MKoa wa Dar es salaam | Ally Awadh (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 14. | Rutala Limited S.L.P. 668 Mpanda | Eneo la Kibamba, Manispaa ya Ubungo | Freddy Herbert Price (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |

Mtu yeyote au kikundi cha watu wenye pingamizi kwa mwombaji yeyote wa leseni hapo juu kwamba asipewe leseni, anatakiwa kuwasilisha pingamizi hilo kwa EWURA ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili kupitia anwani tajwa hapa chini.

IMETOLEWA NA

Kaimu Mkurugenzi Mkuu

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)

Ghorofa ya 4, Jengo la PSSSF, Barabara ya Makole

S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania

Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005

Barua pepe: info@ewura.go.tz

Tovuti: http://www.ewura.go.tz

ewura
Energy and Water Utilities Regulatory Authority
ISO 9001:2015 Certified

***KUMB: PPR/2020 - 05/1***

# TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA BIDHAA ZA MAFUTA YA PETROLI KUANZIA JUMATANO, TAREHE 6 MEI 2020

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia Jumatano, Tarehe 6 Mei 2020. Pamoja na kutambua bei hizo, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

(a) Bei za jumla na rejareja za mafuta ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa yaliyopokelewa nchini kupitia **bandari ya Dar es Salaam** zimepungua ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 1 Aprili 2020. Kwa mwezi Mei 2020, bei za rejareja za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimepungua kwa Shilingi 219/lita (sawa na asilimia 10.50), Shilingi 143/lita (sawa na asilimia 7.17) na Shilingi 355/lita (sawa na asilimia 18.47), mtawalia. Vilevile, ikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimepungua kwa Shilingi 218.59/lita (sawa na asilimia 11.14), Shilingi 142.25/lita (sawa na asilimia 7.63) na Shilingi 354.09/lita (sawa na asilimia 19.69), mtawalia.

(b) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya Petroli na Dizeli katika mkoa wa Tanga zimebadilika ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 1 Aprili 2020. Kwa mwezi Mei 2020, bei za rejareja za Petroli na Dizeli kwa **Mikoa ya Kaskazini** (yaani Tanga, Arusha, Kilimanjaro na Manyara) zimepungua kwa Shilingi 463/lita (sawa na asilimia 21.88) na Shilingi 377/lita (sawa na asilimia 18.21), mtawalia. Aidha, kwa kulinganisha na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli na Dizeli zimepungua kwa Shilingi 461.82/lita (sawa na asilimia 23.19) na Shilingi 375.82/lita (sawa na asilimia 19.33), mtawalia. Bei za Mafuta ya Taa kwa Mikoa ya Kaskazini zitaendelea kuwa zile zilizochapishwa katika toleo la tarehe 1 Aprili 2020 kwa sababu hakuna shehena ya bidhaa hiyo iliyopokelewa nchini kupitia bandari ya Tanga kwa mwezi Aprili 2020.

(c) Kwa mwezi Mei 2020, bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya **Dizeli katika Mikoa ya Kusini (yaani Mtwara, Lindi na Ruvuma)** hazitabadilika ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 1 Aprili 2020 kutokana na kuwa hakuna shehena ya Dizeli iliyopokelewa kupitia bandari ya Mtwara. Hata hivyo, bei za mafuta ya Petroli zimepungua ikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita. Kwa mwezi Mei 2020, bei za jumla na rejareja za Petroli zimepungua kwa Shilingi 129/lita (sawa na asilimia 5.67) na Shilingi 128.14/lita (sawa na asilimia 5.99), mtawalia. Kwa kuwa hakuna Mafuta ya Taa katika bandari ya Mtwara, wamiliki wa vituo vya mafuta katika mikoa tajwa wanashauriwa kununua mafuta hayo kutoka Dar es Salaam na hivyo bei za rejareja za Mafuta ya Taa kwa mikoa hiyo zinatokana na gharama za mafuta hayo kutokea Dar es Salaam na kusafirishwa hadi mkoa husika.

(d) Mabadiliko ya bei za mafuta katika soko la ndani yanatokana na mabadiliko ya bei za mafuta katika soko la dunia na gharama za usafirishaji (BPS Premium) kama inavyoonekana katika **Jedwali C na Jedwali D.**

(e) EWURA inapenda kuukumbusha umma kwamba bei kikomo za mafuta kwa eneo husika, zinapatikana pia kupitia simu za mkononi kwa kupiga namba ***152*00#** na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.

(f) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.

(g) **Kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi tu bei hizo zisivuke bei kikomo (price cap)** kama ilivyokokotolewa na kanuni (formula) iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapishwa katika Gazeti la **Serikali Na. 74 la tarehe 7 Februari 2020.**

(h) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei nafuu zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.**

(i) Wauzaji wa mafuta ya petroli wanatakiwa kutoa risiti za mauzo kutoka kwenye mashine za EFPP (Electronic Fiscal Pump Printers) na Wanunuzi wahakikishe wanapata stakabadhi hizo za malipo zinazoonyesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hizo za malipo zitatumika kama kidhibiti kwa wanunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya aidha kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo au kuuziwa mafuta yasiyo na kiwango cha ubora kinachofaa, na pia, risiti hizo zitasaidia kurahisisha ukusanyaji wa kodi za Serikali zitokanazo na mauzo ya mafuta ya petroli.

**JEDWALI A: BEI ZA REJAREJA**

| Mji | Bei Kikomo | | |
|---|---|---|---|
| | Petroli (Shs/Lita) | Dizeli (Shs/Lita) | Mafuta Ya Taa (Shs/Lita) |
| **Dar es Salaam** | **1,868** | **1,846** | **1,568** |
| **Arusha** | **1,711** | **1,750** | **2,044** |
| Arumeru (Usa River) | 1,711 | 1,750 | 2,044 |
| Karatu | 1,729 | 1,768 | 2,062 |
| Longido | 1,722 | 1,761 | 2,055 |
| Monduli | 1,716 | 1,755 | 2,049 |
| Monduli-Makuyuni | 1,721 | 1,760 | 2,054 |
| Ngorongoro (Loliondo) | 1,795 | 1,834 | 2,128 |
| **Pwani (Kibaha)** | **1,873** | **1,851** | **1,572** |
| Bagamoyo | 1,879 | 1,857 | 1,579 |
| Bagamoyo (Miono) | 1,910 | 1,888 | 1,610 |
| Chalinze Junction | 1,882 | 1,860 | 1,582 |
| Chalinze (Msata) | 1,887 | 1,865 | 1,586 |
| Kibiti | 1,889 | 1,867 | 1,588 |
| Kisarawe | 1,875 | 1,853 | 1,575 |
| Mkuranga | 1,878 | 1,856 | 1,578 |
| Rufiji | 1,896 | 1,874 | 1,595 |
| **Dodoma** | **1,927** | **1,905** | **1,627** |
| Bahi | 1,934 | 1,912 | 1,634 |
| Chamwino | 1,922 | 1,900 | 1,622 |
| Chemba | 1,954 | 1,932 | 1,653 |
| Kondoa | 1,960 | 1,938 | 1,659 |
| Kongwa | 1,924 | 1,902 | 1,624 |
| Mpwapwa | 1,928 | 1,906 | 1,628 |
| Mtera (Makatopora) | 1,946 | 1,924 | 1,646 |
| **Geita** | **2,034** | **2,012** | **1,733** |
| Bukombe | 2,023 | 2,001 | 1,722 |
| Chato | 2,055 | 2,033 | 1,754 |
| Mbogwe | 2,072 | 2,050 | 1,771 |
| Nyang'hwale | 2,049 | 2,027 | 1,748 |
| **Iringa** | **1,932** | **1,910** | **1,632** |
| Ismani | 1,938 | 1,916 | 1,637 |
| Kilolo | 1,937 | 1,915 | 1,636 |
| Mufindi (Mafinga) | 1,942 | 1,920 | 1,642 |
| Mufindi (Igowelo) | 1,951 | 1,929 | 1,651 |
| **Kagera (Bukoba)** | **2,084** | **2,062** | **1,783** |
| Biharamulo | 2,058 | 2,036 | 1,758 |
| Karagwe (Kayanga) | 2,100 | 2,078 | 1,800 |
| Kyerwa (Ruberwa) | 2,106 | 2,084 | 1,806 |
| Muleba | 2,084 | 2,062 | 1,783 |
| Ngara | 2,072 | 2,050 | 1,771 |
| Misenyi | 2,092 | 2,070 | 1,792 |
| **Katavi (Mpanda)** | **2,076** | **2,054** | **1,776** |
| Mlele (Inyonga) | 2,096 | 2,074 | 1,795 |
| Mpimbwe (Majimoto) | 2,069 | 2,047 | 1,769 |
| Tanganyika (Ikola) | 2,094 | 2,072 | 1,794 |
| **Kigoma** | **2,100** | **2,078** | **1,799** |
| Uvinza (Lugufu) | 2,112 | 2,090 | 1,812 |
| Buhigwe | 2,089 | 2,067 | 1,788 |
| Kakonko | 2,057 | 2,035 | 1,756 |
| Kasulu | 2,086 | 2,064 | 1,785 |
| Kibondo | 2,064 | 2,042 | 1,764 |
| **Kilimanjaro (Moshi)** | **1,700** | **1,739** | **2,033** |
| Hai (Bomang'ombe) | 1,704 | 1,743 | 2,037 |
| Mwanga | 1,693 | 1,732 | 2,027 |
| Rombo (Mkuu) | 1,717 | 1,756 | 2,050 |
| Same | 1,687 | 1,726 | 2,020 |
| Siha (Sanya Juu) | 1,707 | 1,746 | 2,040 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Lindi** | **2,152** | **2,196** | **1,627** |
| Lindi-Mtama | 2,157 | 2,201 | 1,645 |
| Kilwa Masoko | 2,176 | 2,220 | 1,602 |
| Liwale | 2,188 | 2,232 | 1,648 |
| Nachingwea | 2,172 | 2,216 | 1,656 |
| Ruangwa | 2,178 | 2,222 | 1,658 |
| **Manyara (Babati)** | **1,745** | **1,784** | **2,078** |
| Hanang (Katesh) | 1,755 | 1,794 | 2,088 |
| Kiteto (Kibaya) | 1,760 | 1,799 | 2,093 |
| Mbulu | 1,758 | 1,797 | 2,091 |
| Simanjiro (Orkasumet) | 1,777 | 1,816 | 2,110 |
| **Mara (Musoma)** | **2,047** | **2,025** | **1,746** |
| Musoma Vijijini (Busekela) | 2,088 | 2,066 | 1,787 |
| Rorya (Ingirijuu) | 2,056 | 2,034 | 1,755 |
| Rorya (Shirati) | 2,091 | 2,069 | 1,790 |
| Bunda | 2,038 | 2,016 | 1,738 |
| Bunda (Kisorya) | 2,048 | 2,026 | 1,747 |
| Butiama | 2,044 | 2,022 | 1,743 |
| Serengeti (Mugumu) | 2,093 | 2,071 | 1,792 |
| Tarime | 2,058 | 2,036 | 1,758 |
| Tarime (Kewanja/Nyamongo) | 2,063 | 2,041 | 1,762 |
| **Mbeya** | **1,975** | **1,953** | **1,675** |
| Chunya | 1,985 | 1,963 | 1,685 |
| Chunya (Makongolosi) | 1,999 | 1,977 | 1,699 |
| Kyela | 1,991 | 1,969 | 1,691 |
| Mbarali (Rujewa) | 1,960 | 1,938 | 1,659 |
| Rungwe (Tukuyu) | 1,984 | 1,962 | 1,684 |
| **Morogoro** | **1,893** | **1,871** | **1,593** |
| Mikumi | 1,909 | 1,887 | 1,608 |
| Kilombero (Ifakara) | 1,931 | 1,909 | 1,631 |
| Kilombero (Mlimba) | 1,954 | 1,932 | 1,653 |
| Kilombero (Mngeta) | 1,943 | 1,921 | 1,642 |
| Ulanga (Mahenge) | 1,942 | 1,920 | 1,641 |
| Malinyi | 1,952 | 1,930 | 1,652 |
| Kilosa | 1,912 | 1,890 | 1,611 |
| Gairo | 1,912 | 1,890 | 1,611 |
| Mvomero (Wami Sokoine) | 1,904 | 1,882 | 1,603 |
| Mvomero (Sanga Sanga) | 1,893 | 1,871 | 1,593 |
| Turiani | 1,918 | 1,896 | 1,618 |
| **Mtwara** | **2,138** | **2,182** | **1,640** |
| Nanyumbu (Mangaka) | 2,175 | 2,219 | 1,689 |
| Masasi | 2,155 | 2,199 | 1,666 |
| Newala | 2,159 | 2,203 | 1,672 |
| Tandahimba | 2,152 | 2,196 | 1,665 |
| Nanyamba | 2,152 | 2,196 | 1,665 |
| **Mwanza** | **2,018** | **1,996** | **1,718** |
| Kwimba | 2,036 | 2,014 | 1,736 |
| Magu | 2,027 | 2,005 | 1,726 |
| Misungwi | 2,013 | 1,991 | 1,712 |
| Sengerema | 2,051 | 2,029 | 1,750 |
| Ukerewe | 2,078 | 2,056 | 1,778 |
| **Njombe** | **1,961** | **1,939** | **1,660** |
| Njombe (Kidegembye) | 1,981 | 1,959 | 1,681 |
| Ludewa | 1,999 | 1,977 | 1,698 |
| Makambako | 1,953 | 1,931 | 1,653 |
| Makete | 1,992 | 1,970 | 1,691 |
| Wanging'ombe (Igwachanya) | 1,959 | 1,937 | 1,658 |
| **Rukwa (Sumbawanga)** | **2,041** | **2,019** | **1,741** |
| Sumbawanga Rural (Mtowisa) | 2,041 | 2,019 | 1,741 |
| Kalambo (Matai) | 2,048 | 2,027 | 1,748 |
| Nkasi (Namanyele) | 2,055 | 2,033 | 1,754 |
| **Ruvuma (Songea)** | **2,224** | **2,268** | **1,691** |
| Mbinga | 2,237 | 2,281 | 1,725 |
| Namtumbo | 2,215 | 2,259 | 1,721 |
| Nyasa (Mbamba Bay) | 2,262 | 2,306 | 1,735 |
| Tunduru | 2,189 | 2,233 | 1,750 |
| **Shinyanga** | **1,997** | **1,975** | **1,697** |
| Kahama | 2,011 | 1,989 | 1,710 |
| Kishapu | 2,026 | 2,004 | 1,725 |
| Ushetu (Nyamilangano) | 2,028 | 2,006 | 1,728 |
| **Simiyu (Bariadi)** | **2,039** | **2,017** | **1,738** |
| Busega (Nyashimo) | 2,032 | 2,010 | 1,731 |
| Itilima (Lagangabilili) | 2,042 | 2,020 | 1,741 |
| Maswa | 2,030 | 2,008 | 1,730 |
| Meatu (Mwanhuzi) | 2,037 | 2,015 | 1,737 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Singida** | **1,959** | **1,937** | **1,659** |
| Iramba | 1,971 | 1,949 | 1,671 |
| Manyoni | 1,943 | 1,921 | 1,643 |
| Ikungi | 1,955 | 1,933 | 1,654 |
| Mkalama (Nduguti) | 1,984 | 1,962 | 1,683 |
| **Songwe (Vwawa)** | **1,985** | **1,963** | **1,684** |
| Songwe (Mkwajuni) | 1,992 | 1,970 | 1,691 |
| Ileje | 1,989 | 1,967 | 1,688 |
| Momba (Chitete) | 1,994 | 1,972 | 1,693 |
| Tunduma | 1,989 | 1,967 | 1,688 |
| **Tabora** | **2,023** | **2,001** | **1,722** |
| Igunga | 1,976 | 1,954 | 1,676 |
| Kaliua | 2,042 | 2,020 | 1,741 |
| Ulyankulu | 2,036 | 2,014 | 1,735 |
| Nzega | 1,987 | 1,965 | 1,687 |
| Sikonge | 2,034 | 2,012 | 1,734 |
| Urambo | 2,036 | 2,014 | 1,735 |
| Uyui | 2,024 | 2,002 | 1,723 |
| **Tanga** | **1,654** | **1,693** | **1,987** |
| Handeni | 1,675 | 1,714 | 2,008 |
| Kilindi | 1,690 | 1,729 | 2,023 |
| Korogwe | 1,666 | 1,705 | 1,999 |
| Lushoto | 1,676 | 1,715 | 2,009 |
| Mkinga (Maramba) | 1,661 | 1,700 | 1,994 |
| Muheza | 1,659 | 1,698 | 1,992 |
| Pangani | 1,661 | 1,700 | 1,994 |

## JEDWALI B: BEI ZA JUMLA

| | Petroli (Shs/Lita) | Dizeli (Shs/Lita) | Mafuta ya Taa (Shs/Lita) |
|---|---|---|---|
| DAR ES SALAAM | 1,743.36 | 1,721.06 | 1,444.08 |
| TANGA | 1,529.75 | 1,568.28 | 1,862.19 |
| MTWARA | 2,012.68 | 2,056.15 | - |

## JEDWALI C: SABABU ZA MABADILIKO YA BEI ZA MAFUTA KATIKA SOKO LA NDANI

| Bandari | Maelezo | Petroli | Dizeli | Mafuta ya Taa |
|---|---|---|---|---|
| DAR ES SALAAM | Mabadiliko ya Bei za mafuta katika soko la dunia | Punguzo la Dola 132.479/Tani | Punguzo la Dola 72.49/Tani | Punguzo la Dola 193.563/Tani |
| | Mabadiliko ya gharama za usafirishaji (BPS premiums) | Punguzo la Dola 4.418/Tani | Punguzo la Dola 2.656/Tani | Ongezeko la Dola 1.750/Tani |
| TANGA | Mabadiliko ya Bei za mafuta katika soko la dunia | Punguzo la Dola 244.407/Tani | N/A Punguzo la Dola 189.768/Tani | N/A |
| | Mabadiliko ya gharama za usafirishaji (BPS premiums) | Punguzo la Dola 24.06/Tani | Punguzo la Dola 6.060/Tani | N/A |
| MTWARA | Mabadiliko ya Bei za mafuta katika soko la dunia | Punguzo la Dola 48.275 /Tani | N/A | N/A |
| | Mabadiliko ya gharama za usafirishaji (BPS premiums) | Punguzo la Dola 14.770/Tani | N/A | N/A |

## JEDWALI D: MWEZI HUSIKA WA BEI ZA MAFUTA KATIKA SOKO LA DUNIA

| | Aina ya Mafuta | Shehena ya Mafuta Ilipokelewa Mwezi: | Mwezi husika wa Bei za Soko la Dunia zilizotumika mwezi huu: | Mwezi husika wa Bei za Soko la Dunia zilizotumika mwezi uliopita: |
|---|---|---|---|---|
| DAR ES SALAAM | Petroli | Aprili 2020 | Machi 2020 | Februari 2020 |
| | Dizeli | Aprili 2020 | Machi 2020 | Februari 2020 |
| | Mafuta ya Taa | Aprili 2020 | Machi 2020 | Februari 2020 |
| TANGA | Petroli | Machi 2020 | Februari 2020 | Novemba 2019 |
| | Dizeli | Machi 2020 | Februari 2020 | Novemba 2019 |
| | Mafuta ya Taa | Machi 2020 | Februari 2020 | Juni 2019 |
| MTWARA | Petroli | Aprili 2020 | Machi 2020 | Januari 2020 |
| | Dizeli | Februari 2020 | Januari 2020 | Novemba 2019 |
| | Mafuta ya Taa | N/A | N/A | N/A |

**Eng. Godfrey E. Chibulunje**
**KAIMU MKURUGENZI MKUU**
**EWURA"**

HABARI BUNGENI

# Madalali wa mahakama wazua jambo bungeni






Habari na Augusta Njoji

MBUNGE wa Viti Maalum (CCM), Mariam Kisangi, ameitaka serikali kutoa kauli kuhusu madalali wasiofuata taratibu ambao wamekuwa wakitumia nguvu kuuza au kudai mali za watu walio na mgogoro.

Akiuliza swali bungeni jijini hapa jana, Kisangi alisema mahakama zimekuwa zikitumia madalali kuuza au kudai mali za watu walio na mgogoro na mara nyingi madalali hutumia watu wenye nguvu (mabaunsa) wasiokuwa wastaarabu kuvamia na kuvunja nyumba au kuuza vitu vya watu bila kufuata utaratibu.

"Hali hii inasababisha wanawake kukosa haki zao. Je, serikali inatoa kauli gani kwa madalali wasiofuata utaratibu?" Alihoji.

Kisangi pia aliitaka serikali kusaidia wanawake wanaopeleka mapingamizi mahakamani ili yasikilizwe kwa haraka kwa lengo la kuepuka kudhulumiwa haki zao.

Katika majibu yake kwa mbunge huyo, Wizara ya Katiba na Sheria ilisema uteuzi wa madalali wa mahakama hufanyika kwa mujibu wa kanuni na Tangazo la Serikali (GN) namba 363 la mwaka 2017 ambalo limeainisha sifa za mtu anayefaa kuteuliwa kuwa dalali wa mahakama.

"Madalali wanaoteuliwa hutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa kanuni za madalali na endapo atakiuka masharti hayo atakuwa ametenda kosa na hatua zitachukuliwa dhidi yake," ilisema.

Wizara hiyo ilizitaja hatua hizo kuwa ni pamoja na kupewa onyo, kusimamishwa kufanya shughuli za udalali kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja au kufutwa udalali kwa mujibu wa Kanuni ya 18 ya Tangazo la Serikali (GN) namba 363/2017.

"Endapo dalali yeyote atakiuka utaratibu wa kukamata mali ambayo haikuainishwa katika hati ya ukamataji atakuwa amekiuka utaratibu uliotajwa kwenye kanuni, hivyo kupelekea kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa kanuni hizo," ilisema.

Ilibainisha kuwa ikithibitika mali husika imekamatwa au kuuzwa kimakosa, mali hiyo itarejeshwa kwa mhusika.

"Mahakama kama chombo cha haki, inapotokea wanawake wanaleta mapingamizi, mahakama imekuwa ikiangalia mashauri yao, sawa na mashauri mengine kwa kuzingatia misingi ya sheria na usawa," ilisema.

Wizara hiyo ilisema kwa mashauri yote ambayo yanahitaji kipaumbele cha pekee, mahakama imekuwa ikiyasikiliza na kuyatolea uamuzi haraka.

# Ataka uwanja wa ndege uhamishwe

BUNGE limeelezwa kuwa serikali inatafuta fedha, ili kukarabati Uwanja wa Ndege wa Njombe kwa viwango vinavyokubalika kimataifa, huku mmoja wa wabunge mkoani humo akiitaka serikali iuhamishie eneo lingine.

Hayo yalibainishwa jana na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, ilipojibu swali la Mbunge wa Viti Maalumu (Chadema), Lucia Mlowe.

Katika swali lake, mbunge huyo alisema uwanja huo umejengwa karibu na makazi ya wananchi na hivyo kusababisha kero kubwa kwa wananchi ambao wamekuwa wakitozwa fedha nyingi kwa kukatiza katika uwanja huo.

"Je, serikali ina mpango gani wa kuhamisha uwanja huo katika eneo lingine katika Mkoa wa Njombe na eneo la uwanja wa sasa kutumika kwa matumizi mengine?" Mlowe alihoji.

Katika majibu yake, wizara hiyo ilisema serikali haina mpango wa kuuhamisha uwanja huo kutoka eneo uliko sasa kwa kuwa tayari imeshaanza kuukarabati.

Ilisema uwanja huo ni kama ilivyo kwa viwanja vingi vya ndege nchini, ulijengwa na wakoloni kabla ya uhuru (miaka ya 1940) na kuanza kutumika rasmi mwaka 1945.

Ilisema kwa mujibu wa Sheria za Kimataifa za Usalama wa Anga, hairuhusiwi kiumbe au chombo chochote (mfano



watu, magari, wanyama) kukatiza kwenye viwanja vya ndege.

"Kutokana na makazi ya watu kuendelea kusogelea eneo la kiwanja mwaka hadi mwaka tangu kujengwa kwake na kukosekana kwa uzio wa usalama, kumesababisha watu kukatiza katikati ya kiwanja kinyume cha sheria," ilisema.

Wizara hiyo ilisema ili kuzuia uhalifu huo, hatua kali ikiwa ni pamoja na kutozwa faini zinachukuliwa kwa watu wanaokamatwa wakikatiza uwanjani.

"Katika juhudi za kuepusha athari hizo, serikari ilikijumuisha kiwanja hiki katika upembuzi yakinifu na usanifu wa kina uliofanywa na kukamilika mwaka 2017 kwa fedha za mkopo kutoka Benki ya Dunia uliohusisha pia viwanja vya ndege vingine 10 ili kukikarabati ikiwa ni pamoja na kujenga uzio wa kuzunguka kiwanja," ilisema.

Ilisema lengo la ukarabati wa uwanja huo ni kuuwezesha kukidhi mahitaji ya uwanja wa mkoa utakaopokea ndege za daraja la kati zenye viwango vinavyolingana na vya Bombardier Q400.

"Kazi zitakazohusika katika ukarabati na upanuzi wa kiwanja ni ujenzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege, barabara ya kiungo na maegesho ya ndege kwa kiwango cha lami, ujenzi wa jengo jipya la abiria," ilisema.

Wizara hiyo ilisema kazi nyingine inayofanyika ni ujenzi wa Kituo cha Zimamoto, ujenzi wa barabara ya kuingia na kutoka uwanjani pamoja na maegesho ya magari na ujenzi wa uzio kuzunguka eneo la uwanja ambao utasaidia kuzuia wananchi, kiumbe au chombo chochote kukatiza ovyo katika eneo la uwanja huo.



# Nyumba za mawakili kujengwa kwa awamu

SERIKALI imesema uwezo wa kibajeti utakapoimarika, ujenzi wa nyumba za mawakili wa serikali utafanyika kwa awamu ili kutatua kero ya makazi iliyopo.

Kauli hiyo ilitolewa jana bungeni na Wizara ya Katiba na Sheria ilipojibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Taska Mbogo.

Katika swali lake, mbunge huyo alisema mawakili wa serikali wako karibu kila mkoa nchini, lakini sehemu nyingi wamepanga ofisi na hawana nyumba za kuishi, hivyo wanapanga uraiani.

"Je, ni lini serikali itajenga ofisi za mawakili wa serikali kwenye mikoa yote ya Tanzania? Na je, ni lini serikali itajenga nyumba za kuishi mawakili wa serikali kwenye mikoa yote nchini?" Alihoji.

Katika majibu ya wizara hiyo, ilibainishwa kuwa lengo la serikali ni kuhakikisha inaboresha utendaji kazi wa watumishi wake, hivyo pale uwezo wa kibajeti utakapopatikana, itajenga nyumba kwa ajili ya kada hiyo.

Ilisema mawakili wa serikali wako karibu kila mkoa na wanatekeleza majukumu yao chini ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka.

Ilisema kutokana na ufinyu wa bajeti, hasa fedha za maendeleo zinazotengwa kwa ajili ya ofisi hizo tatu, kumekuwa na tatizo katika upatikanaji wa majengo ya ofisi hizo.

Ilisema ofisi hizo zimekuwa zikilazimika kutumia majengo ya taasisi nyingine za umma au kupanga katika majengo ya watu binafsi.

Hata hivyo, ilisema jitihada zinaendelea kufanyika ili kuhakikisha ofisi zinajengwa kwa awamu katika mikoa yote kulingana na uwezo wa kibajeti.

"Lengo la serikali ni kuhakikisha inaboresha utendaji kazi wa watumishi wake, hivyo, pale uwezo wa kibajeti utakapokuwa vizuri, ujenzi wa nyumba za mawakili wa serikali utafanyika kwa awamu ili kutatua matatizo kwa mawakili hao kupanga nyumba uraiani," ilisema.

Wizara hiyo iliongeza kuwa itasaidia kuboresha utendaji kazi wa mawakili wa serikali kwa kiwango kikubwa.

## Upinzani majeruhi unapoingia mchakato uchaguzi mkuu

Ukurasa 13





Ukurasa 14

## Muungano unavyoboreka raia wataupenda zaidi

siasa
JUMATANO MEI 6, 2020
HABARI BORA NA KAMILIFU
Nipashe

# Balozi Mahiga: Lulu iliyoondoka

**Na Mashaka Mgeta**

INAWEZEKANA watu wengi hawakumjua Balozi Augustine Mahiga kwa undani, kuhusu maisha yake, taaluma na utumishi wake kwa taifa, kikanda Afrika na kimataifa.

Kifo chake kilichotokea alfajiri ya Mei Mosi, mwaka huu nyumbani kwake mjini Dodoma, kimemuibua 'Mahiga mpya' katika fikra za watu, akiwa Mtanzania ambaye wasifu, salamu za rambirambi na mijadala iliyojikita kuanzia ngazi za msingi kwenye jamii hadi kimataifa, vimekuwa sehemu ya kudhihirisha kwamba nchi bado ina watu wanaoweza kuacha alama chanya duniani.

Balozi Mahiga aliyezaliwa Agosti 28, 1945 na kwa mujibu wa taarifa ya Ikulu, kifo chake kimetokana na kuugua ghafla alfajiri ya Ijumaa iliyopita. Rais John Magufuli ndiye aliyetangaza kifo cha Balozi Mahiga, kupitia kwa Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Gerson Msigwa.



Balozi Mahiga akiwa kazini wakati wa uhai wake. **PICHA: MTANDAO**

Kwa masikitiko akamuelezea Mahiga kwamba alikuwa mchapakazi, mwadilifu, mzalendo na mwanadiplomasia mahiri aliyeiwakilisha na kuipigania Tanzania katika nyanja za kimataifa kwa miaka mingi.

"Pamoja na umri wake mkubwa na uzoefu wa kushika madaraka katika nyadhifa mbalimbali za kitaifa na kimataifa, alikuwa mnyenyekevu na mtiifu kwa kila jukumu nililomtuma," ameeleza Rais Magufuli katika salamu zake rasmi za rambirambi.

Rais Magufuli anasema kifo cha Balozi Mahiga kilitokea baada ya kuugua ghafla akiwa nyumbani kwake jijini Dodoma na alifikishwa hospitalini akiwa tayari ameshafariki dunia.

Spika wa Bunge, Job Ndugai, pamoja na mambo mengine anamtaja kama mzalendo wa kweli, aliyeitumikia nchi yake kwa uadilifu mkubwa.

Mbunge wa Kawe kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Halima Mdee, anaguswa na kifo hicho na kwa ufupi akaandika kupitia ukurasa wake wa twitter, "upumzike kwa amani Balozi Mahiga. Ulikuwa mtu mwema sana."

Kwenye Mahojiano na shirika la utangazaji la Uingereza (BBC) kutokea jijini Dar es Salaam, Mbunge wa Kigoma Mjini -ACT Wazalendo, Zitto Kabwe, anasema Mahiga hakuwa mtu mwenye kuweka kinyongo, bali kuitetea hoja yake katika mazingira yanayofikia ukomo wa kuelewana kwa pande husika.

Zitto anatoa mfano wa hoja moja aliyowahi 'kumbana' bungeni, lakini wakati wa mapumziko, Balozi Mahiga alimuita kwenye mgahawa wa bunge na kumpa maelezo ya ziada yaliyomridhisha.

Salamu za rambirambi zimetumwa kwa kutumia ukurasa wa twitter kutoka balozi za Uingereza, Canada, Ufaransa, Sweden na China, miongoni mwa nyingine.

### UTUMISHI UN

Balozi Mahiga hakukumbukwa hapa nchini pekee, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres ni miongoni mwa walioguswa na kifo chake akasema kupitia kwa msemaji wake, "tunahuzunishwa na kifo cha Balozi Mahiga na tunatuma salamu zetu za rambirambi kwa serikali na wananchi wa Tanzania na familia ya marehemu."

Msemaji huyo, Stephane Dujarric, anawaambia waandishi wa habari kwa njia ya video jijini New York, Marekani, kwamba Guterres anamtambua Balozi Mahiga kwamba alikuwa mtumishi wa umma aliyekamilika, mwanadiplomasia aliyejizatiti hata aliposhika wadhifa wa Mwakilishi Maalum wa Katibu Mkuu wa UN nchini Somalia kati ya 2010 hadi 2013.

Kwa mujibu wa Guterres, wakati akihudumu kwenye jukumu hilo, Balozi Mahiga alikuwa na dhima ya msingi katika kusongesha uundwaji wa serikali ya Somalia na kusaidia kukamilisha Katiba ya muda na maandalizi ya uchaguzi nchini humo.

Mbali na uwakilishi huo, Balozi Mahiga alikuwa Mwakilishi wa Kudumu wa Tanzania kwenye UN kati ya 2003 hadi 2010.

Balozi Mahiga pia alifanya kazi katika Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR), akiongoza ofisi zake nchini Liberia, India, Italia, Malta, Vatican na San Marino huku akiratibu shughuli za shirika hilo katika ukanda wa maziwa makuu.

Kwa upande wake, shirika la habari la Uingereza (BBC), linamuelezea Balozi Mahiga kama mmoja kati ya watu wachache ambao wamefanya kazi katika ngazi za juu na awamu zote tano za serikali ya Tanzania, kutoka kwa Rais wa kwanza, hayati Mwalimu Julius Nyerere hadi John Magufuli wa awamu ya tano.

Kwa mujibu wa BBC, licha ya utajiri wake wa maarifa na uzoefu mkubwa ndani na nje ya Tanzania, alikuwa mtu asiyejikweza kwa mamlaka na hivyo kuwa moja ya sababu ya kifo chake kuombolezwa sehemu nyingi duniani.

Mchambuzi wa masuala ya siasa na uongozi nchini, Furaha Dimitri, anasema, taarifa za maisha ya Balozi Mahiga zinatolewa kama tunu iliyokuwa imefichwa, na sasa inaibuliwa kwa manufaa ya nchi.

"Nina hakika vijana wa kizazi cha hivi karibuni hawakuyajua mengi kumhusu Balozi Mahiga hadi mauti yalipomkuta, sasa ni vizuri kama taifa tukajenga mfumo wa kuwatambua watu wa aina yake na kuwatumia ipasavyo badala ya kusubiri hadi mauti yawakute," anashauri.

Dimitri anasema, kifo cha Balozi Mahiga kinaweza kuwa sababu kwa taifa kuweka mfumo wa kuwatambua watu wenye taaluma na uzoefu katika ngazi tofauti, bila kuhusisha tofauti za aina yoyote zilizopo.

"Tunapoijenga nchi, hakuna sababu ya kuwaona hawa wa kule na wale wa huku, sote tunapaswa kuunganisha nguvu zetu na kutumia rasilimali wakiwamo wa aina ya Balozi Mahiga," anasema.

### MAJUKUMU MUHIMU

Mpaka anafariki alikuwa Waziri wa Katiba na Sheria, nafasi ambayo alikuwa akihudumu tangu Machi 2019.

Kabla ya hapo, Balozi Mahiga alikuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki jukumu alilolishika tangu kuapishwa kwa baraza la kwanza la mawaziri la serikali ya awamu ya tano mwaka 2016.

Aliteuliwa kwenye nafasi hiyo baada ya kuteuliwa na Rais Magufuli kama mbunge wa kuteuliwa. Karibuni zilikuwapo habari kuwa alikuwa anajindaa kugombea ubunge Iringa Mjini.

# BURIANI DK. MASUMBUKO LAMWAI

## • Mwalimu, mwanasheria, mwanasiasa wa kudumu

**Na Sabato Kasika**

DOKTA Masumbuko Lamwai amefariki dunia. Tetesi za mitandao, zimepata uthibitisho wa mdogo wa marehemu, Joseph Selasini, Redio East Africa imepata uthibitisho jana asubuhi.

Anayethibitisha hayo, ni Joseph Selesini, ambaye ukiondoa vigezo vingine vya kushabihiana, kimaumbile na majukumu ya kisiasa wanaangukia katika kapu moja hasa nyendo zao za awali.

Katika Kitivo cha Sheria, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) ambako ndiko alikozoa umaarufu wa kwanza, Dk. Lamwai alikuwa na mvuto kwa wanafunzi si wa kitivo hicho pekee, bali kwa ujumla wake pale 'aliposhusha nondo' kwa sauti yake kali kutoka ghorofa la kitivo hicho, iliyofika umbali mrefu kupita kiasi

Ni aina ya hasara nyingine, inayoiangukia UDSM ambayo ni chini ya wiki moja, imepoteza nembo yake nyingine 'mshika chaki' Dk. Augustine Mahiga, aliyezama zaidi katika uhusiano wa kimataifa, Kitivo cha Sanaa.

Ujuzi wa Dk Lamwai, ulipata umaarufu wa kipekee uraiani hasa alipotikisa katika kesi lukuki hasa za kisiasa zinazohusu uchaguzi. Hapo zinaweza kuzungumziwa jimbo la kwao Rombo, na kwa namna ya kipekee ana rekodi ndiye mtetezi aliyemnusuru Maalim Seif Sharif Hamad, katika kesi nzito iliyomkabili huko Zanzibar.

Pia, katika kesi ya uchaguzi jimbo la Temeke pale aliposimama kizimbani dhidi ya Ramadhan Ally Kihiyo, aina ya maswali mazito, magumu na ya papo kwa hapo hapana shaka yalimpandisha chati maradufu mhadhiri huyo wa UDSM.

Mbali na umaarufu wa stadi za utetezi, pia mbwembwe zake za kuzunguka kizimbani, kujidai na sauti yake kali, tai yake anavyoiweka kwa staili ya kipekee, viatu vya 'sandals' na mzigo mkubwa wa kabrasha anaofika nao katika mahakama hata akasaidiwa na vijana wake, ilikuwa raha ya kipekee.

Ikumbukwe ilikuwa ni kipindi ambacho UDSM ilizalisha mawakili 'moto' ambao kazi yao katika mahakama mbalimbali nchini na kwa nafasi ya kipekee Kisutu jijini Dar es Salaam, nyayo za kazi zao ziko wazi, bila kusahau majina kama Dk. Ringo Tenga na marehemu Prof. Michael Wambali.

Mwanzoni mwa miaka ya 1990 vuguvugu la kutaka msukumo wa kuelekea katika Tanzania yenye mfumo wa vyama vingi vya siasa, wanazuoni wa chuo hicho walikuwa moja ya vituo muhimu vya vuguvugu hilo.

Hapo tena ndiyo yanapoibuka majina ya kina Dk. Tenga, Dk. Mwesiga Baregu, Dk. Sengondo Mvungi, bila kumsahau Dk. Lamwai akiwa chanda na pete za vuguvugu hilo walioungana na wenzao wa uraiani, kama mwanasheria Mabere Marando, James Mapalala, Chifu Abdallah Fundikira, Mwinjilisti Kamala Kusupa, Julius Miselya, Balozi Christopher Kassanga, Tumbo na Mchungaji Christopher Mtikila.



Dk. Masumbuko Lamwai enzi ya uhai wake. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

> Mwenyekiti wa CCM kwa wakati huo Rais Benjamin Mkapa, alisifu umahiri wake kuwa ni mtu anayepangua hoja kwa hoja.

Hao wakaungwa mkono na kundi kubwa la vijana wakiwamo waliokuwa masomoni; James Mbatia (Uhandisi), Ludovick Bazigiza (Elimu), Kimaro (Udaktari), Matiku Matare na Mosena Nyambabe. baadhi yao wameshatangulia mbele ya haki.

Kupitia nyendo hizo, timu ilikamilika kupitia kilichoundwa kwa jina la National Commitee for Reconstruction Reform (NCCR) ambayo kimsingi walibatiza kuwa Kamati ya Kitaifa ya Kuleta Mabadiliko ya Kudai Vyama Vingi vya Siasa

Hapo ndipo kazi ya Dk. Lamwai kisiasa ilionekana; chuoni yupo kuandaa vijana kina Mbatia kisiasa, mahakamani yuko sambamba na kesi zinazoangukia suala hilo, harakati za maandamano na mikutano ya kisiasa hata katika uwanja wa Jangwani, jijini Dar es Salaam, Dk. Lamwai nako yuko juu.

Hatimaye mwaka 1992, lengo la harakati zao lilifanikiwa kwa mabadiliko ya katiba kuhusu vyama vingi vya kisiasa. Ilikuwa ni matokeo ya kazi ya ripoti ya kukusanya maoni iliyoongozwa na Jaji Mkuu Francis Nyalali (marehemu).

Itakumbukwa, umachachari wa Dk. Lamwai pia ilijionyesha katika ukumbi wa Nkurumah, UDSM wakati Tume ya Nyalali ilipofika kukusanya maoni ya katika kisima hicho cha wasomi.

Baada ya ruhusa, vyama vingi viliundwa, yeye alibaki katika chama kitokanacho na NCCR kikisajiliwa kwa jina la NCCR-Mageuzi ambako pia walikuwapo wasomi na wanasheria wenzake, Dk. Mvungi, Dk. Tenga na Marando.

Sasa ndipo ushuhuda rasmi wa mwanasiasa Dk. Lamwai, kwani alishaanza kuweka kando chaki, baada ya kuondoka katika taaluma hiyo na akawa Diwani wa Kata ya Manzese Dar es Salaam na hadi kufikia uchaguzi mkuu wa mwaka 1995, akakwea na kuwa mbunge wa jimbo la Ubungo.

Huku akiwa anaendelea na ofisi yake ya uwakili, aliongezea nguvu kwa kuwachukua rasmi wanafunzi wake baada ya kuhitimu sheria, Majura Magafu na Peter Swai, ambao hata katika kipindi cha mafunzo masomoni walipatikana hapo. Ndani ya muda mfupi 'aliwasuka' na wakawa machachari mno mahakamani hasa katika kesi za uchaguzi, ambazo wakati huo zilirindima mno mahakamani.

Baada ya kumaliza kipindi chake cha ubunge, Dk. Lamwai alikabiliwa na misukosuko akajikuta amefungiwa kushiriki uwakili na ofisi yake ikiendeshwa na vijana wake, ambao nao wakatawanyika kwenda kuanzisha shughuli zao za kisheria.

Huku katika siasa, kipindi hicho NCCR- Mageuzi ilikuwa na sintofahamu ya ndani ambayo katika mtazamo wa kina, ilikuwa kati ya vijana na wakubwa wao, wakati huo timu ya vijana akiwa imeimarika zaidi kwa nguvu za ziada kama vile Joseph Selasini, mtumishi wa zamani wa benki na kisha taasisi binafsi.

Mvutano ulikuwa mkubwa katika mkutano wa uchaguzi wa siku mbili katika mwaka 2000 uliofanyika katika Chuo cha Bandari Tandika Dar es Salaam na kuhitimishiwa katika hoteli iliyopo katikati ya jiji, James Mbatia aliunyakua uenyekiti, kuiweka kando safu ya uongozi wa Marando na timu yake kama kina Dk. Lamwai, Daniel Nsanzugwako na Ndimara Ntigambwagwe.

Katika mkutano huo wa uchaguzi uliokuwa na patashika kali sana, Dk. Lamwai alipopewa kipaza sauti, kunena machache, alitamka kwa masikitiko akisema, Selasini na Mbatia ni wadogo zake na hakutarajia wangeenda kinyume naye kisiasa, huku Nsanzugwako kwa fursa kama hiyo, tone la chozi lilionekana.

Haikuchukua muda, yaliposikika mageuzi ya kishindo, Nsanzugwako na Dk. Lamwai kwa nyakati tofauti, walitangaza kujiunga na kule ambako hawakutarajiwa hata kidogo, Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Baada ya muda alikabidhiwa jukumu la kuwa mwanasheria wa chama hicho, huku akiendelea na shughuli zake za uwakili ambazo alikuwa amesharejeshewa.

Mwenyekiti wa CCM kwa wakati huo Rais Benjamin Mkapa, alisifu umahiri wake kuwa ni mtu anayepangua hoja kwa hoja.

Miaka ya baadaye, Dk. Lamwai hakuonekana sana mahakamani kama ilivyokuwa katika zama zile za harakati za mageuzi lakini aliamua kuirudia 'chaki' yake akiongoza Idara ya Sheria katika jukumu la kitaaluma la kuunda wanasheria katika Chuo Kikuu cha Tumaini, Dar es Salaam.

Kwa ujumla, Dk. Masumbuko Lamwai aliyeondoka jana, ana mengi yasiyohesabika katika maisha ya kijamii, lakini kwa upekee maeneo makuu matatu; ualimu, uanasheria na siasa, daima nyayo zake ni ngumu kufutika.

**MUNGU AILAZE ROHO YAKE MAHALI PEMA. AMINA**

UCHAMBUZI

# Upinzani majeruhi unapoingia mchakato uchaguzi mkuu 2020

**Na Sabato Kasika**



Wanachama wa ACT-Wazalendo wakipasha moto mchakato wa kuchagua viongozi, hivi karibuni. **PICHA: ZOTE MTANDAO.**

WAKATI ikisalia miezi mitano ili kufanyika uchaguzi mkuu wa 2020, mchakato wa mchujo ili kupata wanachama sahihi wa kuviwakilisha vyama vya upinzani kwenye uchaguzi huo umeanza.

Baadhi ya vyama hivyo vimeanza kupiga hatua mbalimbali zikiwamo za kuruhusu wanachama wake kutuma mapema maombi ya kutaka kuwania ubunge na udiwani ili wapitishwe katika mchujo maalumu.

Chadema na ACT- Wazalendo ni miongoni mwa vyama hivyo, ambavyo kwa nyakati tofauti vimefanya mchakato wa kupata wanachama, ambao wanaamini hawawezi kuwaangusha.

Januari mwaka huu, Chadema ilifungua pazia kwa wanachama wake wanaotaka kuwania ubunge na udiwani kuandika barua za maombi kwenye maeneo yao ili majina wajadiliwe na vikao maalum.

Mchakato huo ulifungwa rasmi Machi 30 mwaka huu, huku joto likipanda kutokana na wingi wa wanachama waliojitokeza kuwania majimbo yenye wabunge wa chama hicho na hata kata.

John Mrema ni Mkurugenzi wa Mawasiliano na Mambo ya Nje wa Chadema, ambaye anasema, kujitokeza kwa wingi kwa wanachama wa chama hicho kuwa ni nafasi mbalimbali kunaonyesha jinsi gani kinapendwa.

"Mambo yetu tunafanya kwa uwazi, ndiyo maana tukatangaza mchakato huo wanachama wakajitokeza na sasa tumeshafunga rasmi pazia, zinaendelea taratibu nyingine za kufanikisha mchakato huo," anasema Mrema.

Wakati Chadema imeshafikia hatua hiyo, ACT- Wazalendo nao wametangaza utaratibu utakaotumika kupokea watia nia wa nafasi za ubunge na udiwani kupitia chama chicho katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Katibu Mkuu wa ACT-Wazalendo, Ado Shaibu, anasema, chama kitakutana na wadau mbalimbali na kuweka mpango mkakati ya kuwapokea wote wenye nia ya kuwania nafasi za uongozi hasa katika ngazi ya ubunge na udiwani.

"Sisi bado lakini wiki hii ndiyo tutatangaza utaratibu kwa watia nia wa ngazi za ubunge na udiwani kuanza kujitokeza, ili baadaye wapitie kwenye mchakato utakaowezesha kupata wagombea sahihi," anasema Ado.

> Sisi bado lakini wiki hii ndiyo tutatangaza utaratibu kwa watia nia wa ngazi za ubunge na udiwani kuanza kujitokeza, ili baadaye wapitie kwenye mchakato utakaowezesha kupata wagombea sahihi.

## MAJERAHA

Hata hivyo, vyama vya upinzani vimeanza mchakato wa kuingia katika uchaguzi mkuu vikiwa vinauguza majereha ya kukimbiwa na wanachama wake wakiwamo viongozi, wabunge na madiwani.

Ilikuwa ni mwaka 2016 kasi ya wapinzani kurudi au kwenda CCM ilianza taratibu na kadri miezi ilivyokwenda, ndivyo kasi hiyo iliongezeka, huku vyama vikuu vya upinzani vikiathirika zaidi.

Hali hiyo imeendelea kuvikumba vyama hivyo na huenda miezi michache kabla ya uchaguzi mkuu vikakimbiwa, hivyo ni wazi kwamba majeraha ya kukimbiwa yakazidi kuvikumba vyama hivyo.




Wanachama wa Chadema katika moja ya mikutano yao ya ndani.

Ikumbukwe kuwa katika hamahama hiyo, wabunge 10 wakiwamo saba wa Chadema na watatu wa CUF na madiwani 140 kutoka vyama mbalimbali vya upinzani wamejiunga na CCM.

Wote hao wamekuwa na sababu za kufanana, wanadai kukunwa na uongozi wa serikali ya awamu ya tano kwa jinsi inavyofanya kazi ya kuleta maendeleo, hivyo wakaamua waiunge mkono kwa kuhamia CCM.

Uhamaji huo umezusha hisia mbalimbali kutoka kwa wanasiasa huku baadhi wakidai kwamba sasa upinzani unahitaji kufanya uchunguzi wa mienendo ya wanachama wake kimaadili ili kuwapata wale ambao ni sahihi.

Kwamba hatua hiyo itasaidia kuepuka wale wanaotumia upinzani kama kichaka cha kutimiza malengo yao binafsi, bali wanaotambua kuwa upinzani kwao ni falsafa, itikadi, imani na wasioshawishika.

## TUME YA UCHAGUZI

Mbali na majeraha ya kukimbiwa na wanachama na viongozi, upinzani pia una kilio cha kutaka tume huru ya uchaguzi, na vimeendelea kutaka ombi hilo lifanyiwe kazi kabla ya uchaguzi mkuu wa mwaka huu wa 2020.

Katika kilio hicho, lipo pia suala la wasimamizi wa uchaguzi kuwa wakurugenzi wa halmashauri za miji, manispaa na wilaya kwamba wawekwe pembeni kwenye mchakato huo.

Lengo la kilio ni kutaka kuundwa kwa tume huru ya uchaguzi ambayo inakubalika kwa vyama vyote vya siasa kama njia ya kuleta chachu na kukuza demokrasia nchini.

Muundo wa sasa wa tume hiyo umekuwa ukilalamikiwa kutokana na upatikanaji wa viongozi wake, ambapo upinzani unaamini kwamba unasababisha kupendelea upande mmoja.

Mojawapo ya mambo ambayo upinzani unatamani yafanyike ni japo kuweka viraka kidogo kwenye katiba ambayo yatatengeneza mazingira ya kuhakikisha uchaguzi unakuwa huru na wa haki.

Tume huru inayotakiwa ni ile ambayo mwenyekiti na mkurugenzi wake hawateuliwi na rais na pia watendaji wake wakuu katika ngazi za halmashauri wasiwe ni wakurugenzi wa halmashauri.

Katika hilo, Mwenyekiti wa Chadema Taifa, Freeman Mbowe, amewahi kukaririwa na vyombo vya habari akisema, chama kilishamuandikia barua Rais John Magufuli kikimuomba afanye mabadiliko ya sheria yatakayowezesha kuundwa kwa tume huru kabla ya uchaguzi huo.

Kwamba kuna haja ya Rais Magufuli kuunda tume ya maridhiano kwa lengo la kuepusha malalamiko kutoka kwa vyama vya upinzani na wananchi kwa ujumla na kuwa na taifa lenye umoja na mshikamano.

Wakati upinzani ukiwa na ombi hilo, tayari serikali ilishasema kuwa imejipanga kuhakikisha uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 unafanyika katika mazingira ya amani, uhuru na haki.

Aidha, serikali imeshaahidi kwamba wakati ukifika itazikaribisha nchi na taasisi mbalimbali kuja kuangalia uchaguzi ili kujionea jinsi Tanzania inavyokomaa katika nyanja ya demokrasia.

# Muungano unavyoboreka raia wataupenda zaidi

**Na Gaudensia Mngumi**

MAADHIMISHO ya miaka 53 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar yaliyofanyika mwaka 2017, yalikuwa na kiu ya kusikia kile serikali ya Rais John Magufuli, itakachosema kuhusu hatma ya Muungano.

Lakini Rais hakufanya ajizi aliweka bayana kuwa hakuna kitakachouteteresha Muungano na akazizika ndoto za kuunda serikali tatu na fikra za kuufanya uwe wa shirikisho ama wa kimkataba.

Alitangaza hayo katika hotuba yake aliyotoa Dodoma Aprili 2017 na kuweka wazi kuwa wenye nia za kuwa na sura nyingine ya Muungano hawatapewa nafasi hivyo, wauache ukae ulivyo na pia anawahakikishia Watanzania Bara na Zanzibar kuwa ataulinda kwa nguvu zake zote na iwapo atatokea mjanja kutaka kuuvunja ataanza kuvunjika yeye kwanza, kabla hajatimiza azma hiyo.

Kwa hiyo hatataka kusikia habari za kuuvunja, kuufanya wa mikataba, wa serikali tatu au shirikisho kama ambavyo wapo wanasiasa, wasomi na raia wanaotaka kuubadili.

Rais anaonyesha ni jinsi gani Muungano ni wa muhimu zama hizi na anaangalia jinsi ambavyo dunia ya leo inahitaji kuendeleza miungano na kuachana na hisia za kuuchukia ama kuulaumu mtangamano na ushirikiano wa kitaifa na kimataifa.

Hisia za kuwa na umoja si za Tanzania na Zanzibar pekee bali ziko miongoni mwa wananchi wa madola makubwa ambayo yamekomaa kiuchumi, kisiasa na kitekinolojia. Hata hivyo dunia leo inajadili kuwa na mtangamano na ushirikiano wa kikanda kwa mfano , madola makubwa ya Ulaya kama Ujerumani, Ufaransa, Uholanzi na Hispania yanaendelea kujishikilia kwenye Umoja wa Ulaya (EU), licha ya kwamba yana uchumi mkubwa na yanaweza kujitegemea.

Madola ya EU yana sarafu ya Yuro iliyoanza kutumiwa tangu mwanzoni mwa mwaka 2000, wakati hayo yanatokea madola makubwa na yenye uchumi mkubwa ya Ujerumani na Ufaransa pamoja na Uholanzi yaliachia sarafu zake na kuingia kwenye Yuro ili kudumisha umoja na kuwa na fedha yenye nguvu duniani jambo ambalo linatoka sasa ni Yuro kuwa moja ya sarafu zenye nguvu ikichuana na Dola. Pamoja na sarafu nchi hizo zina visa moja iitwayo Schengen Visa, inayotumiwa na nchi zote wanachama wa mataifa hayo.

Yuro moja ni zaidi ya Sh 2,400 za Tanzania wakati Dola nayo ni karibu sawa na kiwango hicho.

Kwa hiyo Afrika chini ya Umoja wa Afrika (AU) inasisitiza suala la mtangamano wa Afrika na kuwa na sarafu moja , soko la pamoja, pasi moja ya kusafiria, Afrika bila mipaka na shirikisho la kisiasa kupitia kile kinachoitwa The Africa We Want au Agenda 2063 ambayo ni suala la mtangamano uliokamilika kwa kila mkubwa wa

Kwa hiyo si suala la Watanzania tena kupinga Muungano na kutaka kuwe na serikali tatu, mara uwe wa mikataba na wengine wakitaka iitishwe kura ya maoni kuamua uondoke ama ubakie.



Waasisi wa Muungano wakichanganya udongo wa Bara na Visiwani ili kuunganisha mataifa hayo. **PICHA: MTANDAO**

> Kiuchumi, kisaikolojia, kijiografia zinazoelekeza ama kuvunja Muungano kwa sababu wanafahamu kinasababisha watu kuukataa au kuukosoa.

Rais Magufuli anaona kuwa dunia ya zama hizi ni ya ushirikiano siyo ya kutaka kubomoa au kutengana, ndiyo maana katika jitihada za kushirikiana Tanzania ni mwanachama wa mtangamano wa Afrika Mashariki, kadhalika yupo kwenye ushirikiano wa Nchi za KUsini mwa Afrika (SADC).

### KUUNGANISHWA KIHISTORIA

Ni wazi kuwa panapokuwa na muungano uwe wa EU au wa Tanganyika na Zanzibar kuna mambo ambayo historia inayaunganisha.

Kwa mfano Ulaya inaunganishwa na kumbukumbu za vita vikuu vya dunia hasa vita vya pili vilivyoangusha dola la Adolph Hitler wa Mjerumani na Uingereza kutwaa enzi. Hayo yalibadilisha sura ya umiliki wa makoloni kwa Tanzania iliyokuwa chini ya Ujerumani ilichukuliwa na Umoja wa Mataifa na kuwekwa chini ya uangalizi wa Waingereza.

EU inaungana ili kulinda na kuepuka uhasama, ikitaka kudumisha amani na kuendeleza mshikamano miongoni mwa wanachama. Huo ni ukweli kwa vile tangu vita hivyo hakujawa na mapigano mengine wala uhasama miongoni mwa wana EU.

Umoja wa EU ni chipukizi linalokomaa zaidi kwa sababu ya kifo cha Jamhuri za Umoja wa Kisovieti zilizokuwa zinaongozwa na Urusi ambazo ziliangukakuanzia 1994. EU kihistoria inafahamu kilichoiua Urusi , hivyo madola haya yanajizatiti kuongeza dhamira ya kudumisha umoja wa Muungano wa Ulaya.

### TANZANIA NA ZANZIBAR

Muungano wa Tanganyika na Zanzibar pia unaunganishwa na historia , utumwa , ukandamizа na unyonyaji wa mabeberu. Mbegu za ushirikiano zimepwanda kihistoria na Mwalimu Julius Nyerere na Abeid Amani Karume wanaunganishwa kwenye kitovu cha machungu ya ubeberu wa Kiarabu akiwamo Tip Tip mfanyabiashara mkubwa wa watumwa anaowatoa Tabora hadi Bagamoyo na kuwauza Zanzibar kama bidhaa nyingine.

Lakini hayo yalifanyika zamani kabla ya 1964, hivyo Karume na Nyerere wanateswa na machungu ya ukandamizaji, uliochagiza kuanzishwa chama cha ASP na TANU kutetea maslahi ya weusi ambao walidharauliwa, kunyanyaswa na kuipuuzwa.

Ikumbukwe Muungano ulilenga pia kuwa na nguvu ya kuendelea kuyalinda mapinduzi ya Zanzibar yaliyomng'oa Muarabu ya ambayo yalihitaji dola lenye msuli kijeshi na usalama wa taifa wenye nguvu ili kuyalinda dhidi ya chokochoko za wanaopinga Serikali ya Wazanzibari (Waafrika badala ya Waarabu).

### KUBOMOA NI HISIA ZA SIASA

Wanachama wa EU wanafahamu umuhimu wa umoja tena wakiangalia Urusi ilivyoparaganyika. Ni wazi kuwa EU inadumu kwa sababu ya misimamo ya viongozi wanaotaka iendelee mmojawapo ni Kansela wa Ujerumani Angela Markel.

Kadhalika Rais Magufuli na Dk Ali Mohamed Shein,wakifuata nyayo za wastaafu Jakaya Kikwete, Benjamin Mkapa na Ali Hassani Mwinyi, kwa Tanzania Bara na Amani Abeid Karume, Dk. Salmin Amour, Idris Abdul Wakili, Ali Hassan Mwinyi na Abdu Jumbe Mwinyi, hawako tayari kuchezea Muungano. Wanayafahamu mazuri ya Muungano na utamu wa kuwa ndani ya ushirika wa dola lenye nguvu Bara na Visiwani

Ni kazi ya wanasiasa kulinda na kupambana na fikra mchanganyiko zikiwamo za kisiasa,

Kiuchumi, kisaikolojia, kijiografia zinazoelekeza ama kuvunja Muungano kwa sababu wanafahamu kinasababisha watu kuukataa au kuukosoa.

### KUVUNJA UMOJA NI LAANA?

Mwalimu Julius Nyerere aliwahi kuonyesha laana inayotokana na ubaguzi na kuvunja umoja , akitoa mfano wa sumu ya ubaguzi inayoambatana na kujitambulisha kwa ukabila na utaifa licha ya kuwa wote ni Watanzania.

Anaonya kuwa iwapo kuna hisia za kujiondoa kwenye Muungano wa Tanganyika na Zanzibar zitaanza kusikika kelele za sisi Wazanzibari, Sisi Wazanzibara, Sisi Wapemba .... Na kauli nyingine za kujitenga. Yote haya hayajengi.

Ukingalia, Sudan ya Kusini ni taifa lililojiondoa kutoka Sudan ya Khartoum, lakini kinachotokea leo naweza kukifananisha na laana ya kujitenga, kuongezeka maafa kama vifo, vinavyotokana na vita vya wenyewe kwa wenyewe, wakimbizi na umaskini miongoni mwa raia wa Sudan Kusini ndicho kinachojiri, bila kusahau vita visivyokwisha.

Ndiyo maana changamoto kama hizi zinawafanya marais wa Tanzania na Zanzibar kuamua kuulinda Muungano na sasa Rais Magufuli anasema atakayetaka kuuvunja anavunjika kwanza.

Wakati Rais anawaonya wenye kiu na ndoto za kuvuruga Muungano wasitamani kufanya hayo, ni wazi kuwa haiwezekani kuuacha ubaki kama msahafu. Watanzania wapewe jukwaa la kuujadili ili kuuboresha, kuukosoa, kuufanya wa wananchi zaidi badala ya viongozi waasisi au wanasiasa.


Zinahitajika juhudi za kuufuatilia mwenendo wa Muungano, kuibua changamoto, kushauri na kuleta mambo mapya yanayoleta tija kiuchumi, kisiasa na kiteknolojia.

### MUHIMU

Kuimarisha Muungano ni jambo jema hivyo ni vyema kuwa na taasisi inayoshughulikia Muungano kikamilifu. Ianzishe utaratibu wa kutumia utaalamu na ubobezi kutoka kwa viongozi watangulizi kuanzia Marais wastaafu wa Bara na Zanzibar, mawaziri viongozi na wakuu, wanasheria wa serikali,wabunge, mgavana wa benki wasomi kushauri jinsi ya kuboresha taasisi hii.

Ofisi hii ya Makamu wa Rais itumie wataalamu na wana siasa kuratibu na kumaliza changamoto kubwa za Muungano, iitoe ufumbuzi na iwe ni jukwaa la kupokea maoni ushauri na miongozi ya kuboresha ushirikiano huu.

Muungano usiwe wa kisiasa zaidi ulinde maslahi ya pande zote, kiuchumi, uongeze furaha kwa Watanzania, waupende na kuuthamini kuwa ni mali yao na si kulazimishwa.





# Akanusha hospitali uhaba vifaa kujikinga corona

Na Renatha Msungu, DODOMA

MGANGA Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma, Dk. Ernest Ibenzi, amesema hospitali yake haina uhaba wa vifaa vya kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona kwa wafanyakazi wake kama inavyo enezwa mitaani.

Dk. Ibenzi aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa kuhusu mazingira ya kazi, miongozo ya utendaji wakati wa mlipuko wa ugonjwa wa corona.

"Hospitali yetu haina kabisa uhaba wa vifaa kwa ajili ya kujikinga na mlipuko wa janga hili la corona, kila siku asubuhi tunagawa barakoa kwa watumishi wote wa hospitali hii," alisema Dk. Ibenzi.

Alisema kutokana na miongozo ya afya na kanuni zilizopo, hospitali hiyo inahakikisha kwamba inakuwa na vifaa vyote vya kujikinga na virusi vya corona kwa ajili ya watumishi wake wote.

Vile vile, Dk. Ibenzi alisema katika kipindi hiki ambacho kuna ugonjwa wa homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya corona (Covid-19), kanuni, sheria na miongozo ya Wizara ya Afya inasimamiwa ilivyo.

Pia katika kukabiliana na janga hilo, alisema hospitali hiyo imepunguza idadi ya watu wanaotembelea wagonjwa tofauti na ilivyokuwa hapo awali na kila mtu anayeingia anatakiwa kuvaa barakoa.

Pia, aliwataka wananchi kuendelea kuchukua tahadhari ili kujikinga na kuwakinga wengine.

Alifafanua kuwa wanafanya hivyo ili kuhakikisha wafanyakazi wanakuwa salama pale wanapoendelea kutoa huduma za kitabibu kwa wagonjwa mbalimbali wanaojitokeza.

"Hakuna sababu ya kupinga kuvaa barakoa wote tunatakiwa kufanya hivyo ili kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona, " alisema Dk. Ibenzi.

Alisema wako katika mapambano ya ugonjwa huo hivyo ni vyema kila mmoja akawa makini na suala hilo.

Hata hivyo Dk. Ibenzi aliwasisitiza wananchi hususani wakazi wa Dodoma kufuata maagizo yanayotolewa na Wizara ya Afya kwa ajili ya kujikinga na ugonjwa wa huo.

**Hospitali yetu haina kabisa uhaba wa vifaa kwa ajili ya kujikinga na mlipuko wa janga hili la corona, kila siku asubuhi tunagawa barakoa kwa watumishi wote wa hospitali hii**

# Madaraja mawili kujengwa kwa bil. 3.4/-

Na Paul Mabeja, DODOMA

KIASI cha Sh. bilioni 3.457 kinatarajiwa kutumia katika ujenzi wa madaraja mawili yanayounganisha Wilaya ya Mpwapwa mjini na maeneo mengine baada ya kusombwa na maji mwezi Machi, mwaka huu.

Madaraja hayo ni Miembeni ambalo linajengwa na Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (Tarura) linalokadiriwa kujengwa kwa Sh. milioni 457 pamoja na daraja la Tanesco linalojengwa na Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroad) kwa shilingi bilioni tatu.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa, Kaimu Meneja wa Tanroad Mkoa wa Dodoma, Salome Kabunda, alisema kuwa tayari wameshaomba fedha kwa ajili ya kujenga daraja hilo na pia wataunganisha na ujenzi wa lami kwenye barabara hiyo.

Kabunda, alisema kwa kuwa hawajui fedha hizo zitatoka lini, waliamua kuanza ujenzi wa barabara ya mchepuko ambayo itatumika wakati wakisubiri fedha kutoka serikalini.

Alisema barabara ya mchepuko ipo kwenye hatua ya umaliziaji kwa kuwa magari madogo yameshaanza kupita.

"Katika daraja ambalo limesombwa na maji barabara hiyo haina lami hivyo tumeomba shilingi bilioni tatu kwa ajili kujenga daraja pamoja na kuweka lami, hatujajua fedha hizo zitatoka lini," alisema.

Meneja wa Tarura Wilaya ya Mpwapwa, Emmanuel Lukumay, alisema walishaomba fedha za dharura Sh. milioni 457 kwa ajili ya kujenga daraja hilo.

Pia alisema huduma mbalimbali za kijamii bado zinaendelea kwa kutumia daraja moja ambalo ni dogo, licha ya kuwa magari yenye uzito mkubwa hayaruhusiwi kupita.

Katika kukabiliana na changamoto mbalimbali katika miundombinu, Tarura imewataka wananchi kutunza mazingira na kuacha tabia ya kufanya shughuli za kibanadamu kwenye maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya hifadhi za barabara.



Kijana akiuza mbwa ili kujipatia riziki katika eneo la Uhindini, jijini Dodoma jana. Mbwa huyo, alimuuza kwa bei ya 20,000/-. PICHA: **PICHA: IBRAHIM JOSEPH.**

# Wakulima ufuta waomba mfumo stakabadhi ghalani

Na Paul Mabeja, DODOMA

WAKULIMA wa zao la ufuta wilayani Kondoa, mkoani Dodoma, wameiomba Tume ya Ushirika nchini kutoa elimu kuhusu mfumo wa stakabadhi ghalani wa soko la zao hilo.

Wakizungumza na Nipashe, wakulima hao walisema kumekuwapo na kero nyingi katika matumizi ya mfumo huo ambao awamu ya kwanza ilianza mwaka 2019.

Mkulima wa zao hilo, Hadadi Omari, alisema wanaingia katika msimu wa pili wa uuzaji zao kwa kutumia mfumo wa stakabadhi ghalani, lakini hawaelewi mfumo huo.

"Tunaomba serikali itusaidie kwa hili, sisi wakulima wa ufuta tunategemea zao hili ili kujikwamua kiuchumi," alisema.

Naye, Kasimu Abdalla, alisema ni vyema waziri aliyetangaza mfumo huo kwenda Kondoa kujadiliana na wakulima kwa kuwa bado hawana uelewa kuhusu mfumo huo na ni moja ya sababu ambayo wakulima hawataki kuutumia mfumo huo kwa sasa.

Diwani wa Kata ya Salanka, Rahimu Salumu, alisema wakulima walipata kero nyingi kwenye msimu uliopita kwa kuwa ndio ilikuwa mara ya kwanza kuutumia.

"Tuliamini kuna changamoto zilitokea na tulihitaji ufafanuzi ili kuzitatua kabla ya kwenda kwenye msimu wa mwaka huu ili yasijitokeze hayo," alisema.

Akizungumzia suala hilo, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, ambaye ni Mbunge wa Kondoa, aliomba serikali kuliangalia suala hilo ili wakulima kuwa na uelewa nao licha ya kuwa ni mfumo mzuri.

"Ombi letu kama watu wa Kondoa, wizara na serikali iwasikilize wananchi wanataka nini hakuna anayekataa ushirika bali tunahitaji elimu ili wananchi waelewe jambo hili, ushauri wangu mimi kama mbunge washirikiane mwaka huu wasitishe jambo hili badala yake watoe elimu," alisema.

Alisema kuna umuhimu wa elimu kuwafikia wananchi na maeneo ya kukusanyia mazao yote yaainishwe kwenye kata na vijiji 84 vya Kondoa, na kusisitiza hakuna anayepinga mfumo huo kwa kuwa utasaidia wakulima kuuza kwa bei yenye tija kwao.

HABARI MBEYA

# Hekta 100 miti vamizi zaondolewa hifadhini

**Na Innocent Ng'oko,** MBEYA

HEKTA 100 za miti vamizi katika Hifadhi ya Taifa ya Kitulo zimeondolewa kwa lengo la kurudisha uoto wa asili na kutunza vyanzo vya maji kutokana na miti hiyo vamizi ikiwamo ya mikaratusi kufyonza maji kwenye vyanzo vya maji.

Kauli hiyo imetolewa jana na Ofisa Uhifadhi wa Hifadhi ya Taifa Kitulo, Susan Tesha, wakati akizungumza na gazeti hili kuhusiana na jitihada zinazofanywa na uongozi wa hifadhi hiyo katika kukabiliana na miti vamizi ndani ya hifadhi hiyo.

Alisema kabla ya hifadhi hiyo kuanzishwa mwaka 2005 eneo hilo la hifadhi lilikuwa linatumiwa na baadhi ya wananchi ambao walipanda miti mbalimbali ikiwamo ya mikaratusi, miwati na mipaini kwa ajili ya mbao na kuni.

Alisema pia eneo hilo lilikuwa likitumiwa na taasisi zingine za serikali katika shughuli mbalimbali, hali ambayo kwa namna moja ilichangia kuathiri mazingira asili ya hifadhi hiyo.

Alisema hifadhi ya Kitulo ni hifadhi yenye mvuto wa kipekee nchini kutokana na kujaliwa kuwa na maua yanayovutia na ndege wa aina mbalimbali, ambao huhama na kurudi pamoja na hali ya hewa nzuri ambayo humfanya kila mtu kuvutiwa anapotembelea.

"Hifadhi hii imejizolea umaarufu sana na watu wengi wanaotembelea na wengi wa watalii wameibatiza jina la 'bustani ya Mungu' kutokana na kuwa na mvuto wa kipekee wa uwapo wa maua mazuri, maporomoko ya maji na hali ya hewa nzuri," alisema.

Alisema kuna mipango endelevu ya kuboresha uoto wa asili na kuongeza vivutio vya kitalii kwa lengo la kuhakikisha eneo hili linakuwa ni moja ya hifadhi za taifa zenye mvuto zaidi kwa watalii wa ndani na nje ya nchi.

Alisema jitihada za kutokomeza miti vamizi ndani ya Hifadhi ya Kitulo ni endelevu na zinafanywa kwa jitihada binafsi za Hifadhi ya Taifa ya Kitulo na baadhi ya wadau ambao wanashirikishwa kwa ajili ya kuondoa miti hiyo.

Alisema uongozi wa Hifadhi ya Taifa ya Kitulo unaendelea na mikakati ya kuikata miti vamizi na kuweka dawa kwa lengo la kuhakikisha miti yote vamizi inaondolewa kabisa na kuacha eneo hilo katika uoto wake wa asili.

Alisema mbali na jitihada za kuiondoa miti hiyo, kumekuwa na msaada kutoka kwa baadhi ya mashirika, likiwamo Shirika la Wildlife Conservation Society (WCS) ambalo limekuwa na mchango mkubwa ambapo kati ya mwaka 2007 hadi 2017 shirika hilo lilikuwa na mradi maalum wa kutokomeza miti vamizi.

Alisema kuwa hekta 100 zilizokatwa miti hiyo ni sawa na asilimia 25 tu ya eneo ambalo miti hiyo vamizi imeathiri hifadhi hiyo na kuwa kwa sasa uongozi wa hifadhi hiyo unaendelea kuwashirikisha wadau mbalimbali katika kutokomeza miti hiyo vamizi ndani ya hifadhi.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila (wa pili kulia), akiwa ameongozana na baadhi ya wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa huo, kukagua ujenzi wa mitaro ya maji machafu katika stendi ya mabasi ya Tarafani Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi hivi karibuni. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

# Mikakati ya kitaalamu corona yaimarishwa

**Na Innocent Ng'oko,** MBEYA

OFISI ya Mganga Mkuu Mkoa wa Mbeya imesema kuna mikakati madhubuti ya kitaalamu iliyoimarishwa katika kukabiliana na maambukizi ya virusi vya corona kuanzia ngazi ya mkoa hadi mtaa.

Imesema wananchi wanapaswa kuzingatia kila maelekezo ya kitaalamu yanayotolewa.

Hayo yalibainishwa na Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Salumu Manyatta, wakati akizungumza na Nipashe kuhusiana na mikakati iliyowekwa na ofisi yake katika kukabiliana na kuenea zaidi kwa maambukizo ya virusi vya corona.

Dk. Manyatta alisema kabla na baada ya kubainika kwa maambukizo ya virusi hivyo, ofisi yake ilishaweka mikakati madhubuti ya kitaalamu ya kuhakikisha wananchi wanakabiliana ipasavyo kuzuia maambukizo, na ilishatoa elimu kwenye mikusanyiko ikiwamo makanisa na misikitini.

Alisema kuna kamati maalum ya kufuatilia magonjwa na mambo ya afya katika ngazi ya mkoa, na kamati hiyo inaongozwa na ofisa afya ngazi ya mkoa na mpaka sasa hatua zinazofanywa na kamati hiyo ni nzuri na zinalidhisha.

Alisema timu za aina hiyo zipo hadi ngazi za halmashauri, kata na katika vijiji, na kuna viongozi wa vijiji wanashirikiana na wataalamu kuwaelimisha wananchi jinsi ya kujikinga na virusi, ikiwamo kuvaa barakoa na kunawa maji kwa sabuni.

"Tumefanikiwa kutoa elimu hii katika ngazi zote hadi vijijini, na ukienda huko kuna mwitikio mkubwa wa wananchi kuchukua tahadhari maeneo ya vijijini... wengi wao wameanza kuvaa barakoa kutokana na wajasiriamali kuziuza kwa bei nafuu ya kati ya Sh. 500 hadi 1,000," alisema.

Aliziomba halmashauri zote za Mkoa wa Mbeya kwa kushirikiana na wataalamu wa afya kutoa elimu kwa mafundi chereheni kuzingatia ushonaji wa barakoa zenye kuzingatia ubora, na kuwa ni vyema barakoa hizo zikawa na vitambaa viwili.

# Vyama vya ushirika vyahudumia 229,000

**Na Innocent Ng'oko,** MBEYA

JUMLA ya wateja 229,000 wamekuwa wakihudumiwa na vyama vya ushirika mkoani Mbeya kwa lengo la kujiongezea kipato kutokana na fursa mbalimbali ambazo wamekuwa wakipata zikiwamo za usimamizi bora wa soko la mazao yao.

Hayo yalielezwa jana na Mrajisi Msaidizi wa Vyama vya Ushirika mkoani Mbeya, Angela Maganga, wakati akizungumza gazeti hili kuhusiana na hali ya ustawi wa ushirika mkoani hapa kwa vyama vya ushirika.

Alisema Vyama vya Msingi vya Kilimo na Masoko (AMCOS) ambavyo vimekuwa vikisimamia mazao kama kakao, tumbaku na kahawa, vimekuwa na mchango mkubwa katika kusimamia masoko ya uhakika ya wakulima katika soko, hivyo kuleta manufaa ya kiuchumi kwa wakulima wanaouza mazao yao.

Akitolea mfano kwa zao la kokoa, Angela alisema bei ya zao hilo imepanda kutoka Sh. 1500 hadi kufikia Sh. 5,000 hadi sasa kutokana na wakulima wengi kujenga utamaduni wa kuuza zao hilo kwenye vyama vya ushirika.

"Hadi kufikia Desemba 2019 wakulima waliweza kuuza kakao kwenye vyama vyao vya ushirika na kupata kiasi cha Sh. bilioni 59.8 na kuwa wengi wa madalali wameanza kuacha kazi hiyo ya udalali kutokana na kutokuwa na manufaa," alisema Angela.

Alisema zao la tumbaku mpaka sasa kuna vyama 17 vya ushirika na kuwa kwa msimu wa mwaka jana jumla ya kilo milioni 11 ziliuzwa kupitia vyama hivyo vya ushirika na kuwa kiasi cha Sh. bilioni 40 zilipatikana na kugawiwa kwa wakulima hao.

Alisema uwapo wa vyama vya ushirika umekuwa ni mkombozi mkubwa kwa watu wengi hususan wakulima kutokana na kuwapo kwa changamoto ya wakulima wengine kuuza mazao yao kwa madalali ambao wamekuwa wakinunua mazao kwa bei ya dezo ambayo yamnufaishi mkulima.

Alisema mkoa wa Mbeya una jumla ya Saccos 212 ambazo zina hisa za Sh. bilioni 16, akiba kiasi cha Sh. bilioni 19 na Amana kiasi cha Sh. bilioni tano.

Alisema mikopo iliyotolewa kwenye Saccos hizo ni kiasi cha Sh. bilioni 64 na kuwa kati ya mikopo hiyo iliyotolewa kuna kiasi cha Sh. bilioni 40 ambazo zimerejeshwa mpaka sasa.





# Mufti aagiza Maimamu hadhari dhidi ya corona

**NaRahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAIMAMU wametakiwa kutii agizo la Ofisi ya Mufti katika utaratibu mzuri unaofaa wa kufanya ibada katika kipindi hiki cha janga la corona, ikiwamo kuweka nafasi ya mita moja na nusu na wale ambao watashindwa kutekeleza amri hiyo wametakiwa kufunga misikiti.

Hayo yalisemwa na Katibu wa Mufti, Shekhe Khalid Ali Mfaume, alipofanya ziara katika misikiti mbalimbali ukiwamo kwa Bi Ziredi, Mabluu na Shauri Moyo na kuona utekelezaji wa agizo la ofisi hiyo la kuwataka Waislamu kuacha nafasi ya mita moja na nusu wakati wa kufanya ibada.

Alisema utaratibu huo ni wa dharura na unakubalika kwa ajili ya kujikinga na ugonjwa hatari wa corona ambao ni janga la kimataifa.

Alisema nchi mbalimbali za Kiislamu ikiwamo Mecca katika msikiti mtakatifu, ibada inayofanyika hapo ya sala mbalimbali ni kuacha nafasi ya mita zaidi ya mbili.

"Ofisi ya Mufti imewataka Maimamu wa misikiti kutekeleza agizo la kuweka nafasi mita moja na nusu katika kipindi cha kufanya ibada ili kuepuka ugonjwa wa corona...utaratibu huo unatumika katika nchi mbalimbali za Kiislamu," alisema.

Mfaume alitoa agizo na kusema Maimamu ambao watashindwa kutekeleza agizo hilo watalazimika kufunga misikiti au kuwaachia wengine wafanye ibada.

"Hilo ndiyo agizo la Ofisi ya Mufti... Maimamu ambao watashindwa kutekeleza agizo la kuweka nafasi katika nyakati za ibada ni bora kuifunga misikiti hiyo au kutafuta imamu mwengine na kuendelea na shughuli za ibada," alisisitiza.

Naye Imamu wa Msikiti wa Mabluu, Said Ali, aliipongeza Ofisi ya Mufti kwa kutoa elimu ambayo imesaidia kuwaelimisha waumini na kukubaliana na utaratibu wa kuacha nafasi wakati wa kufanya ibada.

"Tumeelimika na elimu iliyotolewa na Ofisi ya Mufti na sasa waumini wote wamefahamu na wapo tayari kutekeleza agizo la kuacha nafasi wakati wa kufanya ibada," alisema imamu huyo.

Awali viongozi wa msikiti huo walitofautiana na wafuasi wao, hivyo kulazimika kufungwa hadi Ofisi ya Mufti na viongozi wake walipofika na kutoa elimu na hatimaye kutatua mgogoro huo.

Baadhi ya Maimamu na waumini wake wametofautiana katika utaratibu mpya wa kufanya ibada uliotolewa na Ofisi ya Mufti katika kipindi hiki cha janga la ugonjwa wa corona, ambapo Waislamu wamezoea kufanya ibada kwa njia ya kushikana sehemu ya mabega pamoja na vidole vya miguu.

Maimamu na waumini wengine wanaamini kwamba kitendo cha kuacha nafasi zaidi ya mita moja na nusu wakati wa kufanya ibada kinachukuliwa ni batili katika ibada hiyo kwani ni sawa na kutoa nafasi kwa shetani au ibilisi kupita na kuvuruga sala hiyo.



Meneja wa Tawi la Benki ya Stanbic Tanzania Mbeya, Hemedi Sabuni (wa tano kushoto), akikabidhi matangi na vitakasa kwa Ofisa Uchumi wa Halmashauri ya Mbeya, Saad Ahmad Mtambule (wa nne kulia) katika ofisi za halmashauri jana. Benki hiyo, imetoa msaada huo ikiwa ni mchango wake katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa COVID-19. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wavuvi wapania kupata mavuno zaidi ya pweza

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAVUVI wa Kijiji cha Marumbi na Uroa wanakusudia kuanzisha utaratibu wa kufunga na kufungua pweza katika maeneo ya mwambao huo ili kuwawezesha kupata mavuno mengi kwa wakati mmoja.

Mkuu wa diko la uvuvi la kijiji cha Marumbi Wilaya ya Kati, Soud Abdallah, alisema wanakusudia kuzungumza na majirani zao kijiji cha Uroa kuweka utaratibu wa kufunga na kufungua pweza kwa ajili ya kuwawezesha kupata mavuno mengi.

Alisema wamevutiwa na wavuvi wa rasi ya Michamvi Wilaya ya Kati ambao mwezi uliopita walifungua uvuvi wa pweza, baada ya kufunga kwa zaidi ya miezi mitatu na kupata mavuno mengi.

"Tunakusudia kuanza kuweka utaratibu wa kufunga na kufungua uvuvi wa pweza kwa miezi mitatu ili kuwawezesha wavuvi kupata mavuno mengi na kujipatia kipato kikubwa," alisema.

Mvuvi wa pweza katika kijiji cha Marumbi, Mwajuma Punguza, alisema utaratibu huo ni mzuri ambao zaidi ya miaka kumi ulikuwa ukitumika na kusaidia kuwawezesha kupata kipato kikubwa.

"Utaratibu huu tunaukaribisha kwa sababu utatusaidia sisi wavuvi wa pweza kupata kipato kikubwa na hivyo kusaidia kufanya shughuli zetu za maendeleo," alisema.

Mkuu wa Hifadhi ya Minai Kanda ya Wilaya ya Kati Unguja, Mohamed Ussi, alisema utaratibu wa kufungia uvuvi wa pweza kwa miezi mitatu ni mzuri ambao hutoa nafasi ya kukua kwa viumbe hao na wavuvi kupata kipato kikubwa.

"Tumekubaliana wakati wowote tunatarajia kutangaza kufunga uvuvi wa pweza kwa miezi mitatu ili kutoa nafasi ya ukuaji wake na hatimaye wavuvi kupata kipato kikubwa wakati wa uvunaji wake," alisema.

Wavuvi wa Kijiji cha Michamvi Wilaya ya Kati mwezi uliopita, waliruhusu wavuvi kuvuna pweza baada ya kuzuia uvuaji wake kwa zaidi ya miezi mitatu na kujipatia kipato kikubwa.

Utaratibu wa kufungia uvuvi wa pweza hufanyika kwa miezi mitatu, ambapo wavuvi hawatakiwi kuvua au kufanya shughuli zozote katika eneo lililotengwa lenye matumbawe na mwamba wenye mawe ambayo ndiyo makazi ya pweza.

# Wawakilishi CCM kusambaza barakoa za mil. 33/- majimboni

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi wa Kamati ya CCM, wameamua kutenga jumla ya Sh. milioni 33 katika mfuko wao kwa ajili ya kutengeneza barakoa na kuzisambaza katika majimbo kwa wananchi kujikinga na maambukizo ya virusi vya corona.

Hayo yalisemwa na Makamu wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi, wakati akizungumza na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambao ni wajumbe wa kamati ya mfuko wa maendeleo wa wawakilishi ofisini kwake.

Alisema kamati ya wajumbe wa Baraza la Wawakilishi miongoni mwa majukumu yake ni kuona jamii ambao ndiyo wapigakura wanakuwa salama wa afya zao, hatua ambayo itawawezesha kushiriki maendeleo ya uchumi.

Balozi Iddi alisema njia za kupambana na ugonjwa wa corona na kupunguza maambukizo yake katika baadhi ya sehemu au majimbo ya uchaguzi ni kuvaa barakoa.

"Nimefurahishwa na moyo wa kamati ya Baraza la Wawakilishi ya Chama Cha Mapinduzi katika kuunga mkono juhudi za serikali dhidi ya mapambano ya ugonjwa huu, ndiyo wajibu wa wawakilishi wa majimbo ya uchaguzi," alisema.

Alisema fedha hizo ni mbali ya fedha zilizotolewa na kamati ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kutoka CCM ya Sh. milioni 50 kwa ajili ya kusaidia mapambano dhidi ya corona.

Naye Mnadhimu wa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wa CCM, Ali Salum Haji, alisema miongoni mwa majukumu ya wawakilishi ni kusaidia matatizo na maendeleo ya wapigakura wanapokabiliwa na majanga yanayotishia maisha yao.

Aliwataka wananchi kuchukua tahadhari dhidi ya corona, ambayo ni janga la kimataifa na kwa nchi zilizoendelea imesababisha maafa makubwa.

Alisema katika mapambano ya ugonjwa huo, wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wameshachangia zaidi ya Sh. milioni 83, zikiwamo milioni 50 zilizotolewa kukabiliana na mapambano hayo.

"Sisi wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kutoka katika Chama Cha Mapinduzi tutaendelea kuchangia fedha katika mapambano dhidi ya corona, na kuhakikisha unatokomezwa.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA KAZI

**WANAHITAJIKA WAFANYAKAZI**

Wanahitajika wasichana wa kuuza Duka na wa kazi za ndani , Wanahitajika haraka sana. Piga Simu namba : **0715 431528 au 0784 431528**


***NIPASHE NI JIBU LAKO***

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676**


## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**KHAISAN HUSSEIN ABDALLAH** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 154 ALF TOYOTA LANDCRUISER. Chassis namba HZJ800013481.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya polisi: DAR/SEL/RB/355712/2020.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JUSTINIAN ANATOL REHUMBIZA anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 182 BCB LANDROVER.**

**Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.**

Taarifa ya Polisi: KAG/BUK/RB/335688/2020.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**AYUBU HASSAN MWALIM** anatangaza kupotelewa na kadi ya Tractor yenye namba za usajili T 507 AFL aina ya SCANIA.

Engine: 4105699

Chassis: 4350087.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **SON/TUN/RB/347536/2020.**

## KUPOTELEWA KWA KADI YA PIKIPIKI.

**Mikila Buruba Adili** mkazi wa kijijicha Ng'wang'wali katika Halmashauri ya mji wa Bariadi Mkoani Simiyu anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki nyumbani kwake ,pikipiki hiyo ni aina ya Toyo yenye namba za uasajili MC 447 AMD. Injini namba KELKE 200003771.

Hivyo yeyote atakayeiona kadi hiyo aipeleke taarifa katika kituo chochote cha polisi kilichopo Mjini Bariadi.

Taarifa ya kupotea kwa kadi hiyo, imetolewa katika kituo cha polisi cha Bariadi kwa namba. **BAR/RB/1124/2020.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**JAPHET A. MBWIGA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili T 263 BND TOYO. Chassis namba KEFKE600000777.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **DAR/KAW/RB/203969/2020**

**MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA MBEYA**
**SHAURI NO.330/2018**
**LENT HUGH KANNONYELE::::::::::::::::::MDAI**
**DHIDI YA**
**ALFRED ANDONDILE FUMBO::::::::::::::MDAIWA 1**
**YONO AUCTION MART & CO.LTD::::::::MDAIWA 2**
**SCULT TANZANIA LTD ::::::::::::::::::::::MDAIWA 3**

**YAH : KUITWA SHAURINI**

KWA : 1.ALFRED ANDONDILE FUMBO
2.YONO AUCTION MART & CO.LTD
3.SCULT TANZANIA LTD

Fahamu kwamba Lent Hugh Kannonyele amefungua shauri dhidi yenu katika baraza hili.

Shauri limepangwa kutajwa tarehe 13/05/2020 saa 2:30 asubuhi mbele ya Mh.T.Munzerere Mwenyekiti wa baraza.

Mnatakiwa kuleta utetezi wa maandishi ndani ya siku 21 tangu tarehe ya tangazo hili.

Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya baraza la Ardhi na Nyumba Mbeya.

Mnaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa ninyi wenyewe au wawakilishi wanaoruhusiwa kisheria.Ofisi za baraza zipo ndani nya eneo la Sabasaba Mbeya mjini.

Kumbuka:Musipo hudhuria siku hiyo baraza litatoa amri stahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo ninyi kuwepo.
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na Lakiri/Muhuri wa baraza hili leo tarehe 14/04/2020.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika Mahakama ya Mwanzo DODOMA MJINI**

**Usimamizi wa mirathi 32/2020**

Ombi la FAIZAN NIZAR LADAK kuteuliwa Msimamizi wa mirathi Marehemu **JAFFERALI HAIDERALI LADAK KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA TANZANIA BARA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnano tarehe 13/5/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa

Tarehe 1/5/2020

## KADI YA GARI IMEPOTEA

SIMBA MTOTO TRANSPORT LTD anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T.719 AGE aina ya SCANIA. Yenye chasis namba 1194696 na Engine namba 3011451.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

TAARIFA YA POLISI: TAN/RB/355492/2020.

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**SAIDI RASHIDI OMARY** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili MC 291 ADM TVS KING. Chassis namba MD6M14PK3E4C60286.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya polisi: DAR/KAW/RB/203972/2020**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**CMG INVESTMENT LIMITED** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T. 445 ACD Toyota Landcruiser Chaisis namba HJ60028381 na engine namba 2H1100273 Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Taarifa ya polisi: BAB/A.23/VOLxvii/2370


**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Kenya kufanya majaribio chanjo corona

**NAIROBI,** Kenya

WANASAYANSI wa Kenya wameungana na wenzao wa kimataifa katika juhudi za kutafuta chanjo ya ugonjwa wa virusi vya corona, kwa kufanyia majaribio dawa tatu.

Majaribio ya chanjo hizo itafanyiwa kwa binadamu ili kubaini ikiwa dawa hizo zinaweza kutibu ugonjwa huo.

**DAWA HIZO NI ZIPI?**

Watafiti hao wamekuwa mbioni kupata idhini ya kufanyia majaribio ya dawa aina tatu ikiwa ni pamoja na:

Remdesivir, ambayo iliidhinishwa na Marekani kama dawa ya dharura ya kutibu ugonjwa wa corona.

Nyingine ni dawa ya kutibu malaria ya hydroxychloroquine, Pamoja na Lopinavir/ritonavir, ambayo pia inatumiwa na wagonjwa wa HIV.

Kwa mujibu wa Gazeti la Nation nchini Kenya, Mtafiti Mkuu katika uchunguzi huo Dk. Loice Achieng Ombajo, ambaye ni Mkuu wa kitengo cha magonjwa ya kuambukiza katika hospitali ya kitaifa ya Kenyatta, alisema kufikia sasa hakuna tiba ya ugonjwa wa virusi vya corona anayopewa mgonjwa.

**Hatua nyingine muhimu kwa mujibu wa watalamu hao, ni kuhamasisha umma kuhusu majaribio hayo ya tiba kabla ya watu kufanya uamuzi ikiwa wanataka kushiriki katika zoezi.**

Alisema badala yake, wagonjwa wanasaidiwa kukabiliana na dalili zinazoonekana kama vile kuwa na homa kali na kuumwa na vidonda vya koo.

"Tuko katika awamu ambayo hatuwezi kubaini moja kwa moja nini kinafanya kazi," alisema Dk. Loice Achieng Ombajo.

Aliongeza kuwa katika majaribio ya tiba wagonjwa wengi wanashirikishwa bila mpangilio maalumu lakini wote wanapewa dawa tofauti na wenzao.

"Kuna uwezekano wa dawa moja ikafanya kazi lakini wataalamu wanatakiwa kufuatilia kwa makini mienendo ya mgonjwa," alisema katika mahojiano na gazeti la Nation.

Alisema hadi kufikia sasa Dk. Ombajo, na wenzake wamepata idhini kutoka kwa kamati ya maadili ya Chuo Kikuu cha Nairobi na mapendekezo yao kuchunguzwa na bodi ya dawa nchini Kenya.

Alisema watafiti hao kwa sasa wanasubiri tamko la mwisho kutoka kwa bodi hiyo na Baraza la kitaifa la Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (NACOSTI).

Alisema hatua nyingine muhimu kwa mujibu wa watalamu hao, ni kuhamasisha umma kuhusu majaribio hayo ya tiba kabla ya watu kufanya uamuzi ikiwa wanataka kushiriki katika zoezi.

Dk. Ombaja alisema kabla ya mtu kushiriki katika majaribio ya tiba, wale wanaoendesha shughuli hiyo lazima watoe maelezo kwa muhusika.

"Kwanza anaambiwa huu ndiyo utafiti tunaofanya, hizi ndizo dawa tunazofanyia majaribio, Hii ndiyo sababu tunazifanyia majaribio, na hivi ndivyo tutakavyokulinda," alisema na kuongeza: "Ukiwa mgonjwa tuna bima ambayo itakuhudumia. Je unakubali kushiriki?,Na endapo mhusika atakubali anapewa fomu ya kutoa idhini. Kisha tunafanya majaribio. Ni mchakato mrefu," alisema Dk. Ombajo.

Wiki moja iliyopita, watafiti kutoka nchini Uingereza walisema wanafikiria kufanyia majaribio ya chanjo ya virusi vya corona nchini Kenya.

Tangazo hilo lilizua ghadhabu miongoni mwa Wakenya ambao walitumia mitandao ya kijamii kupinga hatua hiyo. Shirika la Afya Duniani (WHO) liliwahi kuyaonya mataifa ya Ulaya kwamba bara la Afrika siyo uwanja wa majaribio ya chanjo.

Mkuu wa Shirika hilo, Dk. Tedros Adhanom Ghebreyesus, alilaani kauli alizoziita za kibaguzi kutoka kwa madaktari wawili wa Ufaransa ambao walitaka chanjo ya virusi vya corona kufanyiwa majaribio barani Afrika.

Alisema: "Afrika siyo na haitakuwa uwanja wa majaribio ya chanjo yoyote". **BBC**

## Waliofariki kwa corona duniani wafikia 250,000

**WASHINGTON,** Marekani

IDADI ya watu waliofariki kwa ugonjwa wa virusi vya corona duniani imefikia 250,000.

Hiyo ni kwa mujibu wa Chuo Kikuu cha Johns Hopkins cha nchini Marekani, kinachofuatilia kwa karibu data hizo.

Chuo hicho pia kimesema kuwa takriban watu milioni 3.6 wamepata maambukizo ya ugonjwa huo unaosababishwa na virusi vya corona.

Imesema Marekani ndiyo nchi inayoongoza kwa maambukizo na vifo, ambapo watu milioni 1.2 wamekwishaambukizwa nchini humo, huku wapatao 69,000 wakiwa wamekufa kwa ugonjwa huo.

Imesema nchini Ujerumani, walioambukizwa hadi sasa ni watu 166,000, na idadi ya vifo imepanda hadi kufikia 7000.

Takwimu zinazotolewa na chuo kikuu cha Johns Hopkins zinakuwa na idadi kubwa zaidi ya ile ya Shirika la Afya Duniani (WHO) kwa sababu chuo hicho huwa na matokeo mapya kila wakati.

Hayo yanajiri wakati viongozi wa nchi za Ulaya wametoa ahadi kuchangisha Euro bilioni 7.4 kwa ajili ya kufanya utafiti na kutengeneza chanjo dhidi ya virusi vya corona.

Umoja wa Ulaya (EU) umeahidi kuchangia Euro bilioni moja, Ujerumani itatoa Euro milioni 525 na Ufaransa itatenga Euro milioni 500, na Norway imekubali itachangia katika mpango huo. **RFI**



Mojawapo ya kambi ya wakimbizi wa ndani iliyopo eneo la Ituri, Kaskazini Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC). **PICHA: XINHUA**

## Uganda yalegeza masharti 'Lockdown'

**KAMPALA,** Uganda

RAIS wa Uganda, Yoweri Museveni, amesema kuwa kuvaa barakoa ni jambo la lazima nchini humo kuanzia jana, katika kipindi hiki ambacho marufuku ya kutotoka nje inalegezwa.

Hatua hiyo ilitangazwa Jumatatu usiku na kwamba Rais Museveni alihutubia taifa baada ya kumaliza siku 35 za marufuku ya kutotoka nje ama 'lockdown'.

Rais Museveni alisema watu wanaruhusiwa kuvaa barakoa ambazo zimeshonwa kienyeji na vitambaa.

Hata hivyo, kumekuwa na mashaka kutoka kwa wataalamu wa afya juu ya ufanisi wa barakoa za kutengenezwa nyumbani.

Katika hatua nyengine, Rais Museveni amesema kuwa kuruhusu shughuli kuendelea kama awali inabidi kufanyike kwa umakini na mpangilio ili kuzuia virusi kusambaa kwa kasi.

Kwa kuanzia, Rais Museveni aliruhusu maduka ya jumla, karakana za kukarabati magari, maghala kufunguliwa. Pia aliruhusu wafanyakazi wa bima na idadi ndogo ya wanasheria kurejea kazini.

Masharti mengine yaliyosalia ya marufuku ya awali bado yanaendelea mathalani kufungwa kwa mipaka ya nchi, kutoruhusu usafiri binafsi na wa umma, mikusanyiko ya watu na marufuku ya kutotoka nje usiku bado yamewekwa kwa kipindi kingine cha siku 14.

Rais Museveni alisema hatua hizo mpaka sasa zimetoa mafanikio ambayo ni kuzuia kusambaa kwa kasi kwa virusi hivyo.

"Hauwezi kuacha kulala kwa kuota ndoto mbaya. Tutaanza kufunguka taratibu bila ya kuharibu mafanikio yetu. Mafanikio hayo ni wagonjwa 89, waliopona 55 na hakuna kifo hata kimoja," alisema Rais Museveni.

Idadi mpya ya maambukizo kufikia jana asubuhi nchini humo imeongezeka kutoka 89 mpaka 97.

Kati ya wagonjwa hao, Waganda ni 57. Mpaka kufikia Jumatatu, madereva 30 wa malori walikuwa wamekutwa na corona nchini humo, kati yao Wakenya 13 na Watanzania 12.

Hatua ya Uganda kulegeza masharti ya marufuku hizo yanaendana na Rwanda na Nigeria ambazo kuanzia jana asubuhi zilifanya hivyo. **BBC**



# DYBALA: NIMELIKOSA SANA SOKA DIMBANI

**TURIN,** Italia

NYOTA wa Juventus, Paulo Dybala amesema hakufikiria kama siku moja 'atamisi' sana soka kama ilivyo wakati huu wa mlipuko wa virusi vya corona.

Ligi ya Serie A ilisimamishwa tangu Machi kutokana na ugonjwa wa COVID-19, huku michezo duniani kote ikizuiwa kuendelea.

Dybala awali alipimwa na kukutwa na virusi vya corona, na nyota huyo wa kimataifa wa Argentina ameelezea namna alivyopata uzoefu wa kukabiliana na ugonjwa wa COVID-19.

Huku sasa serikali ya Italia ikiwa imewaruhusu wachezaji kurudi kwenye klabu zao Jumatatu ili kuangalia uwezekano wa msimu wa 2019-20 kuendelea, Dybala ameonyesha matarajio yake ya kucheza soka.

"Nikisema ukweli wangu, kamwe sikuwahi kufikiria nitamisi kucheza soka na kufanya mazoezi," alisema Dybala wakati wa mahojiano kupitia mtandao wa Instagram.

"Nahisi kama nahitaji kufanya mazoezi, kuwaona wachezaji wenzangu na marafiki angalau kugusa mpira kwa sababu kufanya mazoezi nyumbani peke yako hainogi.

"Nahitaji kuvaa viatu vyangu, kukimbia na kufunga mabao... kama mara zote ninavyosema ukiwa na mahaba na kile unachokifanya, unafanyia mazoezi mara kwa mara."

Akielezea kuhusu kupatwa na virusi vya corona, Dybala amesema awali alikuwa na woga sana, lakini kwa kuwa hakuwa akihisi mabadiliko yoyote mwili wake akajikuta akichukulia kawaida.

"Mwanzo niliogopa sana na mpenzi wangu, lakini baadaye nikazoea na kuchukulia kawaida tu," alisema.

# Manchester United, PSG zamgombea Ndidi

**LONDON,** England

KLABU ya Manchester United imeingia kwenye mbio moja na Paris Saint German kuwania saini ya Wilfred Ndidi wa Leicester City.

Miamba hiyo ya Ulaya inataka saini ya mchezaji huyo katika usajili wa majira ya kiangazi msimu ujao.

Ndidi amekuwa kiungo tegemeo wa mabingwa hao wa zamani wa England na msimu huu amecheza kwa kiwango bora kiasi cha kuzivutia klabu hizo.

Kiungo huyo anatajwa ni mmoja wa wachezaji wenye mchango mkubwa kwa wababe hao wa King Power, ambao msimu huu wanakula sahani moja na vigogo kwenye msimamo wa Ligi Kuu England wakishika nafasi ya tatu.

Msimu huu, Ndidi mwenye umri wa miaka 23, amecheza mechi 23 kati ya 27 ambazo Leicester City imecheza na wakati huu ambao ligi zimesimama, amekuwa akijifua kujiandaa kumalizia mechi zilizosalia pindi ligi itakaporejea.

Ndidi ambaye mkataba wake unamalizika mwaka 2024, alinunuliwa na Leicester kwa pauni milioni 17 kutoka klabu ya Genk ya Ubelgiji.





# *Karius avunja mkataba Besiktas*

**LIVERPOOL,** England

GOLIKIPA wa Liverpool, Loris Karius "amevunja" mkataba wake wa mkopo wa miaka miwili na Besiktas kutokana na kutokubaliana na malipo ya mshahara wake.

Karius amekuwa na klabu hiyo ya Ligi Kuu ya Uturuki, Super League, tangu Agosti 2018, lakini alitangaza kumaliza muda wake hapo kwa kuposti kwenye Instagram Jumatatu akisema, "ni aibu kufikia mwisho wa namna hii."

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, atarudi pale Anfield akiwa amecheza mechi 67 kwa Besiktas katika mashindano yote.

Aliiripoti Besiktas kwa Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa), mwezi uliopita, ikiwa ni mara ya pili akilalamikia mishahara yake ambayo hajalipwa.

Kuondoka kwa Karius kumehitimisha mpango wa awali ambapo aliripotiwa kwamba angesaini mkataba wa kudumu na klabu hiyo.

"Unatakiwa kujua kwamba, nimejaribu kila kitu kutatua matatizo yangu," alisema Karius katika video hiyo aliyoiposti kwenye mtandao huo.

"Nilikuwa mvumilivu kwa miezi kadhaa nikiiambia bodi mara kwa mara. Kitu kama hicho pia kilitokea mwaka jana.

"Bahati mbaya hawakujaribu kufanya lolote kumaliza tatizo langu na walikataa hata ushauri wangu wa kunilipa nusu."

# Inter Milan washauriwa kumnunua Pogba

**MANCHESTER,** England

PAUL Pogba anatakiwa kuwaniwa na Inter Milan kama wana nguvu ya kifedha, kwa mujibu wa gwiji wa 'Nerazzurri' hao, Giuseppe Bergomi.

Nyota huyo wa Manchester United, Pogba kwa muda mrefu amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka Old Trafford, huku Real Madrid na klabu yake ya zamani ya Juventus ikitajwa kumwania.

Kocha wa Inter Milan, Antonio Conte, ambaye alifanya kazi na Pogba pale Juve, amewachukua wachezaji kadhaa kutoka Ligi Kuu ya England, wakiwamo Romelu Lukaku, Alexis Sanchez, Christian Eriksen na Ashley Young ambao wametua pale San Siro, huku Victor Moses naye alikatisha muda wa kucheza kwa mkopo kule Fenerbahce na kumfuata kocha wake huyo wa zamani wa Chelsea.

Bergomi, ambaye alitwaa taji la Serie A, Coppa Italia na mataji matatu ya Uefa wakati akicheza hapo Inter, anafikiri Pogba anafiti kucheza katika klabu hiyo.

"Kama wana nguvu ya kiuchumi wanaweza kumpata, wanatakiwa kufanya haraka," alisema akiliambia gazeti La Gazzetta dello Sport.

"Ni kweli kwamba hajawa kwenye ubora wake kwa misimu ya hivi karibuni, lakini atarudi kwa nguvu kwa sababu anajua soka vizuri.

"Hatahitaji kuanza kuzoea mazingira. Kutokana na uwezo wake na kipaji alichonacho atazoea haraka sana kwenye Serie A."





# LIVERPOOL YAMSUBIRISHA KWANZA WERNER

**LIVERPOOL,** England

LIVERPOOL imewaomba wawakilishi wa mshambuliaji wa RB Leipzig, Timo Werner muda zaidi wa kuamua kama watatuma ofa ya kumsajili raia huyo wa Ujerumani.

Werner anatarajiwa kuondoka Leipzig kipindi cha majira ya joto kinachokuja, na klabu kadhaa za Ulaya zimeonyesha nia ya kutaka kumsajili.

Hata hivyo, Liverpool ambao walikuwa wanaongoza kwenye mbio za kuwania saini hiyo kwa miezi kadhaa wameonyesha kuwa bado hawapo tayari kufanya hivyo. Na taarifa zaidi zilisema kwamba, walikaribia kukamilisha dili hilo, lakini gazeti la The Guardian limeripoti kwamba bado kuna safari ndefu, kwani Liverpool bado haijafanya maamuzi yoyote kuhusu usajili wa mchezaji huyo kipindi cha majira ya joto kinachokuja.

'Wekundu' hao wanataka kwanza kuangalia athari ya mlipuko wa virusi vya corona kama watakuwa wameathirika kifedha ili waamue endapo watatumia kiasi cha pauni milioni 52 kumsajili mshambuliaji huyo ama la.

Mazungumzo ya awali kuhusu mkataba yameripotiwa kwamba yalishafanyika, lakini majadiliano ya kina hayawezi kuanza hadi Liverpool itakapopeleka ofa maalumu kwa Leipzig juu ya mpango wao wa kumsajili mchezaji huyo ambaye kwenye mkataba wake kuna kipengele cha kuruhusiwa kuondoka kwa pauni milioni 52.

# *Kalou asimamishwa, kisa dharau corona*

**BERLIN,** Ujerumani

KLABU ya Hertha BSC imemsimamisha Salomon Kalou, baada ya mshambuliaji huyo kuposti video ikioonyesha akivunja sheria ya kujitenga kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Kalou aliposti video kwenye ukurasa wake wa mtandao wa kijamii wa Facebook akipeana mikono na wachezaji wenzake wa Hertha na kuvuruga utaratibu wakati wakifanyiwa uchunguzi wa kiafya.

Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, ina matumaini ya kuendelea mwezi huu baada ya kusimama tangu Machi mwaka huu.

Hertha ilitoa taarifa kupitia kwenye tovuti yake ikisomeka: "Kutokana na video aliyoposti, Salomon Kalou amevunja sheria ya kujikinga na virusi vya corona na klabu haikubaliani na jambo hilo.

"Hivyo basi, Hertha BSC imemsimamisha kufanya mazoezi na kutoshiriki katika hatua yoyote ya michezo."

Kocha wa Hertha, Michael Preetz alisema: "Kwa video ya Salomon Kalou si tu ameharibu taswira ya Hertha BSC, lakini amevunja sheria ya serikali kuhusu kujikinga na virusi vya corona."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# XAVI: MESSI ANAWEZA KUCHEZA NA MIAKA 39

## Anajitunza sana na ana uhakika atacheza michuano ya Kombe la Dunia nchini...

**BARCELONA,** Hispania

LIONEL Messi anaweza kucheza soka hata akikaribia umri wa miaka 40, kwa mujibu wa mchezaji mwenzake wa muda mrefu wa Barcelona, Xavi.

**Mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or mwenye umri wa miaka 32, alikuwa kwenye kiwango cha kuvutia msimu huu kwa Barca, akifunga mabao 24 katika mashindano yote kabla ya mlipuko wa virusi vya corona kusimamisha msimu.**

Messi amekuwa mchezaji muhimu sana kwa mafanikio ya Blaugrana hao na Xavi anahisi kwamba nyota huyo wa Argentina bado ana muda wa kutosha kupata mafanikio zaidi katika ngazi ya klabu na kimataifa.

"Bado ana miaka mizuri mitano au saba ya kuendelea kucheza," alisema Xavi akimzungumzia Messi wakati wa mahojiani mubashara kupitia kwenye Instagram na mshambuliaji wa zamani wa Barca, Samuel Eto'o.

"Anajitunza sana na anaweza kuendelea kucheza hadi akiwa na umri wa miaka 37, 38 au 39.

"Atacheza michuano ya Kombe la Dunia nchini Qatar, nina uhakika."

Kama Messi atakuwa na nafasi ya kukaa muda mrefu zaidi klabuni hapo, Xavi anaweza kumnoa kama kocha wa klabu hiyo.

Kocha huyo wa klabu ya Al Sadd alifanya mazungumzo na klabu yake hiyo ya zamani mapema mwaka huu kabla ya Quique Setien kuteuliwa kuchukua mikoba ya Ernesto Valverde aliyefukuzwa.

"Januari, haukuwa muda sahihi," alisema Xavi, akielezea kwa nini aliikataa nafasi hiyo mapema mwanzoni mwa mwaka huu.

"Nilikuwa na majadiliano na Eric Abidal (Mkurugenzi wa soka wa Barcelona) na Oscar Grau (Ofisa Mtendaji Mkuu wa Barcelona) na walinipa ofa kubwa, lakini haukuwa muda sahihi.

"Nahitaji muda zaidi wa uzoefu. Kuinoa Barcelona ni ndoto zangu. Ningependa kufanya hivyo siku moja. Nishasema mara nyingi."

Pia, Xavi amebainisha angependa kuona Neymar akirudi kutoka Paris Saint-Germain na kuwa sehemu ya kikosi hicho.

Mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Brazil mara kwa mara amekuwa akihusishwa na mpango wa kurudi tena pale Camp Nou tangu alipoondoka kwa ada iliyoweka rekodi mwaka 2017.

"Yeye ni miongoni mwa wachezaji watatu bora duniani, bila shaka yoyote," aliongeza Xavi. "Anaweza kutengeneza tofauti.

"Ngoja tuwe na matumaini atarudi Barcelona. Mimi ni shabiki wa Barcelona na nataka wachezaji bora pale."

## ZISIKUPITE

### LIVER YAMSUBIRISHA WARNER

KLABU ya Liverpool wamewaambia wawakilishi wa Timo Warner mwenye umri wa miaka 24, kuwa wanahitaji muda zaidi ili kuamua kama watatuma ofa kwa mshambuliaji huyo wa RB Leipzig. ***(Guardian)***

### MADRID KWA CAMAVINGA

REAL Madrid wanaangalia uwezekano wa kumsajili kinda wa Rennes ya Ufaransa, Eduardo Camavinga mwenye umri wa miaka 17, ambaye pia anawindwa na Manchester United. ***(AS)***

### GOMEZ AGOMBEWA HISPANIA

KIUNGO wa Sao Paulo ya Brazil, Igor Gomez , 21, yupo kwenye rada za Real Madrid, lakini klabu yake haijapokea ofa rasmi. Klabu za Barcelona, Sevilla na Ajax pia zinaripotiwa kummezea mate. ***(Globo Esporte)***

### PARTEY AJIPELEKA ARSENAL

KIUNGO wa Atletico Madrid, Thomas Partey, 26, ameweka wazi kuwa angependelea kuhamia katika klabu ya Arsenal na anaamini makubaliano ambayo yanamhusisha mshambuliaji, Alexandre Lacazette kuhamia Atletico yatafanikiwa. ***(Telegraph)***

### OZIL AWANIWA FANERBAHCE

KLABU ya Fenerbahce ya Uturuki imeripotiwa kuwa katika mipango ya kumsajili kiungo wa Arsenal, Mesut Ozil mwenye umri wa miaka 31, kabla ya mkataba wake kumalizika mwishoni mwa msimu ujao. ***(Sun)***

### REAL NA OFA KWA POGBA

KLABU ya Real Madrid inajipanga kutuma ofa ya kumsajili kiungo wa Manchester United na Ufaransa, Paul Pogba mwenye umri wa miaka 27. ***(Mundo Deportivo)***

### NEYMAR KUKATWA MSHAHARA

NYOTA wa Brazil, Neymar mwenye umri wa miaka 28, bado anataka kuihama PSG na kurejea Barcelona na inaaminika kuwa yupo tayari kukatwa mshahara kwa asilimia 50 ili kutimiza ndoto yake ya kurudi Hispania. ***(Mundo Deportivo)***

### NEWCASTLE KUILIPA SPURS

KLABU ya Newcastle itawalazimu kuilipa Tottenham Hotspur pauni milioni 12.5 kama watataka kumchukua kocha, Mauricio Pochettino mwezi huu, lakini hawatatoa hata fedha yoyote wakimchukua baada ya Mei 31. ***(ESPN)***

### POGBA, LINGARD SOKONI

KLABU ya Manchester United ipo tayari kumuuza kiungo wake, Paul Pogba mwenye umri wa miaka 27, na kiungo wa kati Muingereza Jesse Lingard mwenye umri wa miaka 27, ili kumnunua Sancho. ***(Sun)***

### SANCHO AMTULIZA MKURUGENZI

MKURUGENZI wa michezo wa Borussia Dortmund amesema "amenyamaza " kuhusu hatima ya baadaye ya Jadon Sancho. Winga huyo wa England mwenye umri wa miaka 20, amehusishwa na tetesi za kuhamia Manchester United. ***(Sport1)***

### MOISE ATAKA KUTUA NAPOLI

NYOTA wa Everton, Moise Kean mwenye umri wa miaka 20, amehusishwa na tetesi za kuhamia katika klabu ya Napoli ya Italia. ***(Corriere dello Sport)***

HABARI MICHEZO

## Nahodha Machomane hajasimama na Ligi Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

NAHODHA wa timu ya Machomane ya Ligi Kuu Zanzibar, Seif Ali, amesema licha ya ligi hiyo kusimama, yeye hajawahi kusimama kufanya mazoezi ya mwili jambo ambalo limemsaidia kuendelea kuwa fiti na tayari kwa kurejea dimbani wakati wowote.

Machomane yenye makazi yake Kisiwani Pemba na huu ukiwa ni msimu wao wa kwanza kucheza Ligi Kuu baada ya kupanda daraja msimu uliopita, hadi ligi hiyo inasimama kutokana na mlipuko wa maambukizo ya virusi vya corona, ipo nafasi ya 11 ikiwa na alama 24 baada ya kushuka dimbani mara 21 katika msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 16.

Akizungumza na gazeti hili mapema wiki hii, nahodha huyo alisema anatumia muda mwingi kufanya mazoezi ya mwili pamoja na pumzi ili kuhakikisha anaimarisha mwili wake na kuwa tayari kwa ligi hiyo itakaporejea tena.

Alisema mazoezi anayopendelea kuyafanya kwa siku ni ya kukimbia pamoja na kupiga mpira mara kwa mara ili kuhakikisha hapotezi uwezo wake wa kuuthibiti miguuni mwake.

Alisema kipindi hiki ni kigumu kutokana na ukweli kwamba huwezi kuwakusanya wachezaji wote na kafanya mazoezi ya pamoja, hivyo ni wakati wa kila mchezaji kutumia nafasi yake kwa kufanya mazoezi binafsi ikiwa ni pamoja na kuendeleza programu za mazoezi wanazopewa na walimu wao.

## Alliance yatoa siri wachezaji kujifua

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa timu ya Alliance FC umesema kuwalipa mishahara kwa wakati wachezaji wao ndiyo silaha kubwa kwao katika kufanya mazoezi kwa kuzingatia maelekezo ya benchi la ufundi.

Akizungumza na Nipashe juzi, Meneja wa timu hiyo, James Bwire, alisema wako katika nafasi mbaya katika msimamo hali ambayo imewasukuma kupambana kutafuta fedha ili kuwalipa mishahara wachezaji wao kwa wakati, jambo ambalo wanaamini litawawezesha kuzingatia mazoezi binafsi katika kipindi hiki ambacho wapo mapumzikoni kutokana na mlipuko wa maambukizo ya virusi vya corona.

Alisema anaamini mchezaji anapokuwa nyumbani na hana uhakika wa kupata fedha, inachangia kutofanya mazoezi kwa umakini kama awapo kambini.

"Ni ngumu kumfuatilia mchezaji kuhusu mazoezi, uongozi kazi tuliyokuwa nayo ni kupambana kuwalipa kwa wakati. Unapomlipa mchezaji kwa wakati unaweza kumfuatilia kwa ukaribu kwa sababu hatakuwa na mawazo ya kutafuta pesa zaidi ya kutaka kufanya mazoezi," alisema Bwire.

Alisema licha ya kupambana kutafuta fedha, lakini wamekuwa wakiwafuatilia makocha kwa kuwahimiza kuwasiliana na wachezaji wao, lengo likiwa ni kutaka kujinusuru kushuka daraja.

# NDANDA KUOMBA MSAADA 'TUTANI' TFF

**Na Saada Akida**

WAKATI Bodi ya Ligi Tanzania (TPLB), ikieleza inatarajia Ligi Kuu kurejea rasmi mapema Juni, Katibu Mkuu wa Ndanda FC, Seleman Kachele amesema wanampango wa kuliangukia Shirikisho la Soka nchini (TFF), kuomba kuwezeshwa kiuchumi ili kumudu kushiriki kinyang'anyiro hicho kilichoishia raundi ya 10 kabla ya kusimama Machi mwaka huu.

Ligi Kuu ilisimama Machi 17, mwaka huu kutokana na agizo la serikali la kusitishwa shughuli zote zinazosababisha mikusanyiko ya watu ikiwamo michezo kutokana na mlipuko wa maambukizo ya virusi vya corona (COVID-19) vinavyoitesa dunia kwa sasa.

Hata hivyo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa TPLB, Almas Kasongo, juzi alisema wanatarajia ligi hiyo itarejea mapema Juni endapo watapata baraka kutoka kwa serikali, kauli hiyo akiitoa siku moja baada ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli kusema anafikiria kuruhusu ligi za mpira wa miguu kuendelea nchini.

**Kachele alisema wanajipanga kwa ajili ya kurejea kwa ligi hiyo, ila hofu yao kubwa ni kuyumba kwa uchumi kutokana na ligi kutarajiwa kuanza kuchezwa bila ya mashabiki.**

Alisema wakati wakiwaomba pia wadau wa soka kuwachangia, wanaangalia uwezekano wa kwenda kuomba msaada kwa TFF kuiwezesha timu yao mahitaji muhimu ikiwamo usafiri kutoka kituo kimoja hadi kingine hususan kwa mechi za ugenini.

"Tangu limeibuka hili janga fedha zimekatika, hivyo kila unapokwenda kwa wadau wanakuambia kutokana na bajeti yao wanasubiri hadi ligi itakaporejea, tukipata msaada wa kiuchumi tunaweza kutatua changamoto zote zinazotukabili," alisema Kachele.

Alisema kwa sasa wanazungumza na wachezaji wao, huku wakiwataka kupambana na kutilia mkazo mazoezi ili watakaporejea waisaidie timu yao kubakia Ligi Kuu msimu ujao.

"Kiuchumi hatuko vizuri, hivyo tutakaporejea ufanisi hautakuwa mzuri kama ilivyo kuwa awali kabla ya janga la corona kuibuka," alisema katibu huyo.

Hadi ligi hiyo inasimama Ndanda FC ilikuwa katika nafasi ya 16 ikiwa na alama 31 baada ya kushuka dimbani mara 29.

MAZOEZI...




Baadhi ya wanariadha wakifanya mazoezi katika Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## *Corona yachelewesha 'uhai' Gofu Wanawake*

**Na Saada Akida**

RAIS wa Chama cha Gofu cha Wanawake Tanzania (TLGU), Sophia Reiffenstein, amesema pindi serikali itakaporuhusu michezo kurejea nchini, mikakati yao ni kuhakikisha wanafanikiwa kufufua klabu zote zilizokufa katika mchezo huo.

Serikali ilipiga marufuku shughuli zote zinazosababisha mikusanyiko ya watu nchini tangu Machi 17, mwaka huu, ikiwamo michezo kutokana na mlipuko wa maambukizo ya virusi vya corona, ambavyo vimekuwa tishio duniani kote, huku vikiendelea kuteketeza maelfu ya watu.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, Sophia alisema wanasubiri tamko kutoka serikalini juu ya kuruhusu michezo kuendelea ili waendelee na mchakato wao wa kufufua klabu zote zilizokufa, ambao tayari walishaanza kuufanya.

Alisema hadi sasa wamefanikiwa kufufua klabu moja ya Lugalo ya jijini Dar es Salaam ambayo walifanya uchaguzi wao kabla ya janga la corona na kupata viongozi wapya.

"Sasa hivi Lugalo wanajiongoza wenyewe kwani wao walifanikiwa, ila tunasubiri mwongozo kutoka serikalini juu ya kuruhusu michezo ili tuelekee Moshi, Morogoro, Arusha na Mufindi kwa ajili ya kwenda kufufua klabu za mchezo wetu kwa wanawake," alisema Sophia.

Sophia alisema mbali na mikakati hiyo, lakini wanafikiria kuhakikisha timu ya Taifa ya Gofu ya Wanawake inaenda Namibia kushiriki michuano ya Chalenji Afrika.

Michezo
Jumatano Mei 6, 2020
Nipashe




Xavi: Messi anaweza kucheza na miaka 39 UKURASA 22




Rais wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), Wallace Karia. **PICHA: MAKTABA**

## ZFF yaisikilizia serikali Ligi Z'bar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Bodi ya Ligi ya Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Haji Issa Kidali, amesema kwa sasa wanasubiri muongozo kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili kujua ligi zote zitarejea tena ama la.

Akizungumza na gazeti hili jana, alisema matarajio yao ni ligi hizo kurejea tena dimbani kati ya Juni mwanzoni mwaka huu, endapo tu serikali itatoa muongozo wa kufanya hivyo.

Alisema ana matumaini makubwa serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itatoa tamko juu ya kuchezwa kwa ligi hiyo kulingana na hali watakavyoona kama inaruhusu.

Alisema awali Kamati ya Mashindano chini ya mkurugenzi wake, katibu na baadhi ya wajumbe kwa kushirikiana na Bodi ya Ligi, walikuwa na majadiliano mafupi juu ya hatima ya ligi hiyo ambayo imesimama kutokana na mlipuko wa maambukizo ya virusi vya corona hapa nchini.

"Mwanzo tulikuwa na mambo mawili; aidha, ligi ifutwe au iendelee kuchezwa, lakini pia yote haya yalikuwa yanataka muongozo kutoka serikalini, na matumaini yetu serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Rais wake, Dk. Ali Mohamed Shein kupitia wizara yenye dhamana na michezo itatoa muongozo juu ya kuendelea kwa ligi hiyo, " alisema.

Aidha, aliwataka viongozi wa klabu kuendelea kuwa na subra katika kipindi hiki ambacho wao wenyewe wanashauku ya kujua juu ya hatima ya ligi hiyo na muda uliopo ili kukimbizana na msimu ujao.

# TFF YAZIONYA KLABU KUFANYA MAZOEZI

## ●●● Yataka zisubiri kwanza tamko rasmi la serikali, Kamati ya Tiba na TPLB wajifungia huku...

**Na Mwandishi Wetu**

HUKU likiendelea kusubiri kupata baraka za serikali kuhusu ruhusa ya kurejea kwa ligi nchini, Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), limetoa tahadhari kwa timu zote kutoanza mazoezi ya pamoja hadi hapo tamko rasmi litakapotolewa, imeelezwa.

**Juzi Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi nchini (TPLB), Almas Kasongo, alinukuliwa akisema endapo watapata baraka za serikali wanatarajia ligi hiyo kuanza mapema Juni mwaka huu, lakini jana TFF ikatoa onyo kwa wanachama wake, klabu kutoanza kwanza mazoezi kabla ya serikali kutoa tamko.**

Hata hivyo, TFF imesema bado inaendelea na mchakato wa kurejesha Ligi Kuu Bara, kauli hiyo ikitokana na tamko la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli kwamba anafikiria kwa siku zijazo kuruhusu ligi za mpira wa miguu kuendelea ili angalau watu wawe wanatazama kupitia TV.

Rais Magufuli alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki akiwa Chato mkoani Geita wakati akimwapisha, Dk. Mwigulu Nchemba kuwa Waziri wa Katiba na Sheria kuchukua nafasi iliyoachwa wazi na Marehemu Balozi Dk. Augustine Mahiga, aliyefariki dunia Mei Mosi, mwaka huu, ambapo alisema: "Watanzania tusiwe na hofu, tuendelee kuchapa kazi, wanasiasa waache kutumia hii kama ajenda, haitaweza kuwasaidia, Watanzania lazima tuishi, kwa siku zinazoendelea ninafikiri kuruhusu hata ligi za mipira ziendelee, nasubiri wataalamu wangu wanishauri".

Lakini katika taarifa ya TFF iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari kupitia kwa Ofisa Habari wa shirikisho hilo, Cliford Ndimbo, ilieleza kuwa mchakato wa kurejea kwa ligi hiyo bado ni wa ndani, hivyo wanachama wake wote wanapaswa kuendelea kutekeleza agizo la awali la serikali la kuepuka mikusanyiko ikiwa ni pamoja na kutoanza mazoezi ya pamoja hadi hapo maelekezo mengine yatakapotolewa.

"Pamoja na michakato ya ndani ya TFF na TPLB kuhusu mashindano yake kuendelea, bado hatima ya kurudi kwa mashindano yote itategemea uamuzi wa serikali, ambayo itaelekeza muda muafaka wa kurejea kwa mashindano.

"TFF na Bodi ya Ligi tutatoa maelezo mengine baada ya kupata muongozo wa serikali," ilieleza sehemu ya taarifa hiyo.

Na katika kuhakikisha afya za wachezaji zinazingatiwa endapo watapata baraka za serikali za kurejea kwa ligi hiyo, jana TPLB ilikuwa ina kikao na Kamati ya Tiba ya TFF kupata ushauri wa kitaalamu juu ya namna ligi itakavyoendeshwa kwa kuzingatia tahadhari dhidi ya maambukizi ya virusi vya corona (COVID19) vinavyoitesa dunia kwa sasa, ambapo hadi jioni ya jana jumla ya watu 3,669,747 duniani kote walishabainika kupata maambukizo kati ya hao 1,210,583 wakipona na vifo vikiwa ni 253,169.

Kwa Tanzania pekee jumla ya watu 480 wameshabainika kupatwa na maambukizo kati yao 167 wakipona na vifo vikiwa ni 16.

Kamati ya Tiba ya TFF inaundwa na watu makini, ambapo inaongozwa na Mwenyekiti, Dk. Paul Marealle, Makamu wake akiwa ni Dk. Fred Limbanga huku wajumbe wakiwa ni Dk. Norman Sabuni, Dk. Lisobina Kisongo, Dk. Eliezer Ndama, Dk. Billy Haonga, na Dk. Violet Lupondo.

Hadi ligi hiyo inasimama ilikuwa imebakiza takriban raundi 10 tu kabla ya kumalizika, Simba ilikiwa kileleni mwa msimamo na alama 71, ambazo ni 17 mbele ya Azam FC inayoshika nafasi ya pili, huku Yanga ikiwa ni ya tatu na pointi zake 51, lakini ipo nyuma kwa mchezo mmoja.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >